**KUTOKA KWA: MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA BUKOMBE**

**KWENDA KWA: BARAZA LA MADIWANI**

**TAREHE: 07 DISEMBA, 2020**

**YAH: TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KATIKA KATIKA KIPINDI KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020**

*Mheshimiwa Mwenyekiti* pamoja na Wajumbe wa Baraza la Madiwani, taarifa hii inahusisha Idara zifuatazo:-

1. Idara ya Fedha na Biashara
2. Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu
3. Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji
4. Idara ya Elimu Msingi
5. Idara ya Elimu Sekondari
6. Idara ya Afya
7. Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
8. Idara ya Mifugo na Uvuvi
9. Idara ya Ardhi, Mipango Miji, Misitu na Maliasili
10. Idara ya Maendeleo ya Jamii
11. Idara ya Ujenzi na Zimamoto
12. Idara ya Usafi na Mazingira
13. Kitengo cha Sheria
14. Kitengo cha Tehama
15. Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
16. Kitengo cha Ukaguzi wa ndani
17. Kitengo cha Nyuki
18. Kitengo cha Uchaguzi

**Taarifa ya Fedha Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizovuka mwaka, zilizopokelewa na kutumia katika Kipindi cha Kuanzia Julai hadi Novemba 2020 nikama ifuatavyo;**

**TAARIFA YA FEDHA BAKAA 2019/2020**

***Mhe. Mwenyekiti;***

Hadi Mwaka wa Fedha 2019/2020 unakamilika, jumla ya **Tshs. 1,809,668,811.10** zilivuka mwaka na kuingia mwaka 2020/2021 kwa mchanganuo ufuatao kwenye jedwali Na. 01 hapa chini. Hadi kufikia Novemba, 2020 Jumla ya **Tshs. 530,409,752.52** zimeshatumika sawa na asilimia **29.31**

**Jedwali Na 01: Muhtasari wa Fedha za Bakaa 2019/2020 kuishia 30 Septemba, 2020**

| CHANZO | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | % |
|---|---|---|---|
| **SRWSS** | 175,768,504.80 | 143,230,265.00 | 81.49% |
| **MABOMA YA NYUMBA ZA WALIMU** | 50,000,000.00 | 36,136,000.00 | 72.27% |
| **MFUKO WA MISITU TANZANIA (TaFF)** | 296,770,306.30 | 58,924,042.92 | 19.86% |
| **SWASH-AFYA** | 272,830,000.00 | 177,202,500.00 | 64.95% |
| **EP4R - ELIMU MSINGI** | 720,000,000.00 | 102,375,935.00 | 14.22% |
| **EP4R - ELIMU SEKONGARI** | 294,300,000.00 | 12,541,009.60 | 4.26% |
| **JUMLA** | **1,809,668,811.10** | **530,409,752.52** | **29.31%** |

**TAARIFA YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021**

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha **2020/2021,** Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha **Tshs. 6,949,711,750.98/=** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Miradi ya Maendeleo katika Sekta Mbalimbali. Fedha hizo zilipaswa kutoka katika vyanzo vikuu 4 ambavyo ni Mapato ya ndani, Ruzuku toka Serikali Kuu, Wafadhili na Jitihada za Jamii.

*Mhe. Mwenyekiti;*

Hali ya upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo katika **kipindi cha Kuanzia Julai hadi Novemba 2020** si wa kuridhisha kwani hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2020. Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs. **923,720,789.91** sawa na asilimia **13.29** ya fedha zilizopangwa kwa Mwaka Mzima ambazo ni **Tshs. 6,949,711,750.98/=**. Fedha hizi zilizopokelewa zimetoka katika vyanzo mbalimbali (**TASAF, MDH, Elimu Bure Msingi na Sekondari n.k**)

Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2020 kiasi cha **Tshs. 866,490,877.69/=** kilikuwa kimeshatumika sawa na asilimia **93.80** ya fedha iliyotolewa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali kama **Jedwali Na; 02** linavoonyesha hapo chini.

**Jedwali Na 02: Muhtasari wa Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Maendeleo kuishia 30 Novemba, 2020**

| Na | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA PANGWA | FEDHA TOLEWA | | FEDHA TUMIKA | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | KIASI | % | KIASI | % |
| 1 | Serikali Kuu (MSD) | 571,735,811.00 | - | - | - | - |
| 2 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF) | 670,274,000.00 | - | - | - | - |
| 3 | Malipo kwa Ufanisi (RBF) | 938,394,000.00 | - | - | - | - |
| 5 | LANES | 122,451,000.00 | - | - | - | - |
| 6 | Ruzuku (Sekondari - Elimu Bila Malipo) | 780,822,500.00 | 164,000,112.00 | 21.00% | 164,000,112.00 | 100% |
| 7 | Ruzuku (Msingi - Elimu Bila Malipo) | 1,137,975,537.98 | 245,510,147.58 | 21.57% | 245,510,147.58 | 100% |
| 8 | Programme for Result - P4R | 400,000,000.00 | - | - | - | - |
| 9 | Mfuko wa Jimbo (CDCF) | 55,646,000.00 | - | - | - | - |
| 10 | Global Fund | 9,385,000.00 | 9,261,159.33 | 98.68% | 4,400,000.00 | 47.51% |
| 11 | UNICEF | 10,000,000.00 | - | - | - | - |
| 12 | Mtoto Mwelevu (IMA) | 23,414,102.00 | - | - | - | - |
| 14 | Management Development for Health – MDH | 619,435,600.00 | 123,351,880.00 | 19.91% | 122,579,753.00 | 99.37% |
| 15 | Mapato ya Ndani (40%) | 582,619,200.00 | 145,143,131.00 | 24.91% | 93,657,865.11 | 64.53% |
| 16 | Mfuko wa Hifedhi ya Jamii (TASAF III) | 1,027,559,000.00 | 236,454,360.00 | 23.01% | 236,343,000.00 | 99.95% |
| **Jumla Ndogo Miradi ya Maendeleo** | | **6,949,711,750.98** | **923,720,789.91** | **13.29%** | **866,490,877.69** | **93.80%** |

**Changamoto na Mikakati ya Utatuzi**

***Mhe. Mwenyekiti;***

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto ambazo zinapelekea kutokamilika au kuchelewa kukamilika kwa Miradi mbalimbali ya Maendeleo.

**Jedwali Na; 03 Changamoto na Mikakati ya Kutatua**

| Na; | CHANGAMOTO | MIKAKATI YA KUTATUA |
|---|---|---|
| 1 | Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kuchelewa kutolewa na hivyo kuathiri utekelezaji kama ilivyopangwa. | Jitihada zinafanyika kwa kuwasiliana na Serikali kuu kwa kuwakumbusha juu ya Utoaji wa Fedha hizo. |
| 2 | Mwamuko mdogo wa jamii katika kuchangia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Hii inakwamisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. | Wananchi wanaendelea kuhamasishwa juu ya Uchangiaji katika Miradi mbalimbali ya Maendeleo ilikuweza kukamilika kwa wakati |
| 3 | Fedha zinazotolewa na Vifaa vya Ujenzi vinavyonunuliwa kutokutumika kwa Wakati (Fedha za Bakaa) na hivyo kupelekea Miradi mbalimbali ya maendeleo kutokamilika | Wakuu wa Idara/Vitengo wanaendelea kuhamasihwa kutumia fedha hizo kwa Wakati na kufuata Mpango kazi yao. |

***Mhe. Mwenyekiti;***

Katika kipindi cha Julai, 2020 – Novemba, 2020 Idara hizi ziliendelea na shughuli zake za utendaji wa kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na:-

- Kuandaaa Mpango na bajeti ya Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2020/2021.
- Kusimamia usafi wa mazingira na utoaji huduma za afya.
- Uhamasishaji juu ya upimaji wa hiari na kujikinga dhidi ya Virusi vya UKIMWI.
- Utoaji ushauri kwa wakulima juu ya uhifadhi bora wa mazao, kujiandaa na msimu wa kilimo.
- Kusimamia ujenzi miundombinu katika Sekta ya Afya na Elimu Msingi na Sekondari.
- Kusimamia na kukagua Miradi ya Maendeleo Ngazi ya Kata na Ngazi ya Halmashauri.
- Uandaaji wa taarifa na maagizo mbalimbali kwa ajili ya utendaji kazi wa Halmashauri.
- Kutoa elimu ya ujasiliamali na usajili wa vikundi vya wajasiliamali.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Pamoja na maelezo ya jumla, naomba kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Julai 2020 – Novemba, 2020 kwa Idara tajwa hapo juu, kwa mgawanyo kama unavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

Jedwali Na; 04 Mgawanyo wa Taarifa ya Utendaji Kazi Kiidara


| Na. | Idara/Kitengo | Kurasa |
|---|---|---|
| 1) | Idara ya Fedha na Biashara | 6 – 7 |
| 2) | Idara ya Utawala na Utumishi | 8 – 10 |
| 3 | Idara ya Usafi na Mazingira | 11 – 12 |
| 4) | Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | 13 – 15 |
| 5) | Idara ya Elimu Msingi | 16 - 19 |
| 6) | Idara ya Elimu Sekondari | 20 – 22 |
| 7) | Idara ya Afya | 23 – 29 |
| 8) | Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 30 – 34 |
| 9) | Idara ya Mifugo na Uvuvi | 35 – 37 |
| 10) | Idara ya Ardhi, Mipango Miji Misitu na Maliasili | 38 - 42 |
| 11) | Idara ya Maendeleo ya Jamii | 43 – 48 |
| 12) | Idara ya Ujenzi na Zimamoto | 49 – 50 |
| 13) | Kitengo cha Sheria | 51 – 55 |
| 14) | Kitengo cha Tehama | 56 – 59 |
| 15) | Kitengo cha Ugavi na Manunuzi | 60 |
| 16) | Kitengo cha Ukaguzi wa ndani | 61 – 63 |
| 17) | Kitengo cha Nyuki | 64 – 66 |
| 18) | Kitengo cha Uchaguzi | 67 – 70 |


***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha.

*Dionis M. Myinga*

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**BUKOMBE.**

**TAARIFA YA IDARA YA FEDHA NA BIASHARA KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020.**

## 1.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Idara ya Fedha na Biashara ni moja wapo kati ya Idara 12 na Vitengo 06 zilizopo katika Halmashauri ya Bukombe na Idara hii inajumla ya Watumishi 17.

### 1.1 Muundo wa Idara

Idara ya Fedha na Biashara inaundwa na vitengo vitano ambavyo ni:-

i. Kitengo cha Hesabu za mwisho
ii. Kitengo cha matumizi
iii. Kitengo cha Mapato
iv. Kitengo cha Biashara
v. Kitengo cha Mishahara

#### 1.1.1 Kazi zilizotekelezwa kwa kipindi cha kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2020 hadi Novemba 2020.

i. Ufungaji wa Hesabu za mwaka **2019/2020**
ii. Kuandaa makisio ya Bajeti ya Mapato ya Ndani kwa mwaka **2021/2022**
iii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi yote ya Halmashauri.

### 1.2 Mapato

**(i) Mapato ya Ndani**

Kwa bajeti ya Mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya iliweka malengo ya kukusanya Kiasi cha TZS 1,945,991,292.00 Hadi kufikia tarehe 30/11/2020 jumla ya kiasi cha **TZS 518,307,197.72** kimekusanywa kama mapato hii nisawa na asilimia **25** ya lengo la mwaka ambaoni **TZS 1,945,991,292.00**

**(ii) Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida**

Kwa bajeti ya Mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya iliweka malengo yakupokea Kiasi cha TZS 61,359,928,998.00 Jumla ya kiasi cha **TZS 8,796,039,860.00** kimepokelewa ambapo **TZS 8,051,660,360.00** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS 744,379,500.00** nikwa ajili ya matumizi mengineyo, mapokezi hayo ya fedha sawa na asilimia **14.32** ya lengo la mwaka la **TZS 61,359,928,998.00**

**(iii) Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo**

Kwa bajeti ya Mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya iliweka malengo yakupokea Kiasi cha TZS 6,359,733,124.05 Hadi kufikiatarehe 21/11/2020 jumla ya kiasi cha **TZS 118,986,237.82** cha mapato ya ndani kimehamishwa katika Akaunti ya Miradi ya Maendeleo, ilikutekeleza miradi ya Maendeleo kwa kupitia fedha za

Mapato ya Ndani. Mchango huo ni sawa na asilimia **20.42** ya lengo la mwaka la **TZS. 582,592,200.00**

Kwa bajeti ya Mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya iliweka malengo ya kupokea Kiasi cha **TZS** 6,359,733,124.05 Kwa upande wa miradi ya Maendeleo ya fedha za Ruzuku jumla ya kiasi cha **TZS 775,898,534.02** kimepokelewa hadi kufikia tarehe 31/10/2020, mapokezi haya sawa na asilimia**11.39** ya lengo la mwaka ambaloni **TZS 6,359,733,124.05**

## 1.3 CHANGAMOTO

i. Mwitikio mdogo wa Wananchi katika kulipa kodi/tozo kwa wakati
ii. Wafanyabiashara wenye Mashine za Ki-electronic (EFD mashine) Kutokutoa Risiti
iii. Baadhi ya Wafanyabiashara wakubwa kwa waodogo wenye Kitambulisho vya Wajasiriamali wanakataa kutoa tozo zingine kwa Mfano Ada ya Leseni.
iv. Mkanganyiko wa Sheria ya tozo za Ushuru kwa mazao ya misitu katika ya Halmashauri na Mawakala wa Misitu Tanzania TFS
v. Baadhi ya Hotel na Nyumba za Wageni kutokusajili wateja wote kwenye Vitabu vya mapokezi
vi. Mwitikio mdogo wa Wananchi katika kununua Viwanja eneo la Uyovu
vii. Kutopatikana kwa mfumo wa mapato (utoaji wa bill/ankara) kwa wakati na hivyo kupelekea mapato ya Halmashauri yaliyokusanywa kushindwa kupelekwa benki katika kipindi hicho.

## 1.4 MIKAKATI

i. Kuendelea kutoa elimu kwa walipa Kodi juu ya umuhimu wakulipa kodi kwa wakati
ii. Halmashauri inashirikiana na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) ili kuhakikisha kuwa Wafanyabiashara wote wenye mashine za Ki-electronic wanatumia Mashine hizo.
iii. Halmashauri inaendelea kufanya ukaguzi kwenye hoteli na Nyumba zote za wageni ili kubaini wanaofanya udanganyifu katika kusajili wageni kwenye vitabu.
iv. Halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi kununua viwanja eneo la Uyovu Kata ya Uyovu na Msinila Kata ya Igulwa kupitia vikao vya kata, Mtaa na Vijiji pamoja na Vikao vya Menejimenti ya Halmashauri.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020.**

## 2.0 TAARIFA YA WATUMISHI

### 2.1 UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Idara ya Utumishi ni miongoni mwa Idara 12 na Vitengo 6 vinavyounda Menejimenti ya Halmashauri. Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba Idara imesimamia shughuli mbalimbali za Utawala kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

### 2.2 IDADI YA WATUMISHI

***Mhe. Mwenyekiti***, hadi kufikia mwezi Novemba, 2020 Halmashauri ya Wilaya Bukombe ina jumla ya watumishi 2,116 kati ya watumishi 2,622 wanaohitajika hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 506.

### 2.3 MAENEO YA KIUTAWALA NA VIONGOZI WA KUCHAGULIWA MAENEO YA UTAWALA NA KUTOLEA HUDUMA

***Mhe: Mwenyekiti***, hadi kufikia Novemba, 2020 maeneo ya kutolea huduma kwa Umma na kiutawala ni kama yalivyotangazwa katika Notisi ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) na Amri ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) mwaka 2019 kama inavyosomeka katika jedwali hapa chini:-

**Jedwali Na; 05- HALI YA UTAWALA**

| IDADI YA MAJIMBO | MAMLAKA YA MJI | IDADI YA TARAFA | IDADI YA KATA | IDADI YA VIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | IDADI YA SHULE ZA MSINGI | SHULE ZA SEKONDARI | IDADI YA ZAHANATI | IDADI YA VITUO VYA AFYA | IDADI YA HOSPITALI YA (W) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 3 | 17 | 64 | 348 | 80 | 15 | 9 | 4 | 1 |

### 2.4 MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

***Mhe: Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma 2003 kifungu 128-129 namna inavyoundwa Bodi ya Ajira ya Halmashauri na muda unaotumika kwa kila Bodi inapoundwa. Kwamba kila Bodi itatumika kwa kipindi cha miaka mitano na wajumbe wa Bodi ni kama walivyo ainishwa katika kanuni hiyo.

Hata hivyo mwenyekiti wa Bodi anapatikana kwa ushindani baada ya kutangaza na kuteuliwa na mamlaka ya Serikali za mitaa. Mnamo tarehe 17/8/2020 ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ilitangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ili kujaza nafasi

hiyo kwakuwa Mwenyekiti aliyepo amemaliza muda wake, maombi yaliyo pokelewa baada ya Tangazo hilo ni ya watu wawili tu kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na; 06- MAJINA PENDEKEZWA**

| S/N | JINA KAMILI | WASIFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | EDWARD S MAKALA | Ana ufahamu wa masuala ya kiutumishi, utawala na uongozi alikuwa mwenyekiti wa bodi ya ajira bukombe kuanzia 2015-2020 | Aliteuliwa kuendelea kwa kuwa alimudu kazi yake awali vizuri |
| 2 | LADISLAUS MUGARULA | Ana ufahamu wa masuala ya kiutumishi, utawala na uongozi | |

## 2.5 WATUMISHI WALIOBADILISHIWA MUUNDO

***Mhe. Mwenyekiti*** watumishi wafuatao walibadilishiwa muundo baada ya kujipatia sifa za kimuundo kwa kujiendeleza na watumishi hao wameshabdailishiwa muundo na kikao cha bodi ya ajira kilichoketi tarehe 17/07/2020

## 2.6 JEDWALI NA; 07 - WATUMISHI WALIOSTAAFU KAZI

| NA | JINA LA MTUMISHI | CHEO | IDARA | MWEZI WA KUSTAAFU KAZI | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CANDIDA A NJUNWA | MWALIMU | E/MSINGI | JULAI | Ameondolewa kwenye mfumo |

## 2.7 JEDWALI NA; 08 - WATUMISHI WALIOHAMA/HAMIA

| NA | JINA LA MTUMISHI | CHEO | IDHINI YA UHAMISHO | KITUO CHA AWALI | KITUO KIPYA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | NESTORY MADAHA | MUUGUZI MKUU | RAS GEITA | BUKOMBE DC | GEITA MJI |
| 2. | GATI MAHIRI | AFISA MUUGUZI MSAIDIZI | TAMISEMI | BUKOMBE DC | BUNDA MJI |
| 3. | DAYS S SHAEM | AFISA MUUGUZI | TAMISEMI | KOROGWE DC | BUKOMBE DC |
| 4 | WALTER P NDIMBO | AFISA UGAVI MWANDAMIZI | RAS GEITA | BUKOMBE DC | CHATO DC |
| 5 | OTIENO ASSA | AFISA USTAWI WA JAMII | TAMISEMI | BUKOMBE DC | TABORA MC |
| 6 | NKWIMBA MHANDA | MWALIMU | TAMISEMI | BUKOMBE DC | KAHAMA MJI |
| 7 | BERNADETHA MIHAMBO | MSANIFU MAJENGO | TAMISEMI | BUKOMBE DC | NJOMBE MJI |

**2.8 KUTHIBITISHWA KAZINI WATUMISHI**

Mhe Mwenyekiti, nawasilisha majina ya watumishi walio ajiriwa 1/9/2019 walio timiza muda wao wa kuthibitishwa kazini kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za mwaka 2009 kifungu. Na. D.45 (1) na D.40 (1) Watumishi waliothibitishwa ni kama ifuatavyo;-

**Jedwali Na; 09- WATUMISHI WALIOTHIBITISHWA**

| S/N | JINA LA MTUMISHI | CHEO | TAREHE YA AJIRA | TAREHE YA KUTHIBITISHWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | HIDAYA SHABANI | WEO II | 01/09/2019 | 01/09/2020 |
| 2 | ASIA NJALIKAI | WEO II | 01/09/2019 | 01/09/2020 |
| 3 | BEATRICE VITALIS | WEO II | 01/09/2019 | 01/09/2020 |

**2.9 UNUNUZI WA VITI UKUMBI WA HALMASHAURI**

Mhe. Mwenyekiti, miongoni wa majukumu ya idara ya Utawala na Utumishi ni Pamoja na kusimamia majengo ya Halmashauri Pamoja na mali zilizopo, hii ni Pamoja kushauri matengenezo yanapotakiwa kufanyika na uboreshaji wa ofisi. Idara ilishauri menejimenti ukumbi upakwe rangi na kununuliwa viti na meza kwa kuwa hakuna viti ukumbini kabisa viti vilivyopo ni vya kata ya Igulwa.

**2.9 TAARIFA YA WATUMISHI WENYE MASHAURI YA NIDHAMU NA WATUMISHI WENYE KESI MAHAKAMANI**

Mheshimiwa Mwenyekiti watumishi wenye mashauri ya nidhamu na kesi Mahakamani hadi kufikia mwezi Novemba, 2020 ni kama ifuatavyo;-

**Jedwali Na; 10- ORODA YA WATUMISHI**

| NA | JINA LA MTUMISHI | CHEO | MASHTAKA YALIYOMKABILI | KESI NAMBA | HATUA ZILIZOFIKIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mary Mgula | Muuguzi | WIZI WA DAWA | hajapandishwa kizimbani kesi ipo polis | upelelezi umekamilika jalada limepelekwa kwa mwanasheria wa serikali |
| 2 | Clara Jonathan Kway | Mwalimu shule ya Msingi Lyamba mgongo | KUTUMIA CHETI CHA MTU (IMPERSONIFICATION) | shauri lipo mamlaka ya nidhamu | Anatumia cheti cha ndugu yake. |
| 3 | Dr Bahati Msige | Daktari II | UTORO KAZI | ametumiwa shtaka ajieleze kwanini mtoro kazini | Alifukuzwa kazi kwa utoro kazini |

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha;

## TAARIFA YA IDARA YA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA TAREHE JULAI HADI NOVEMBA 2020.

### 3.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Shughuli za Idara ya mazingira katika Halmashauri ya Bukombe ni Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Katika kusimamia sheria ya Mazingira Idara inafanya shughuli zifuatazo

- Udhibiti wa Taka Ngumu.
    - Kukusanya taka ngumu na kuzisafirisha kuzipeleka dampo katika maeneo ya Mitaa, Kata, Vijiji na Vitongoji. Zoezi hili linafanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi.
    - Utozaji tozo za Usafi
- Usimamizi wa Mazingira kwenye Miradi ya Maendeleo na Shughuli za binadamu ili kuzuia Athari kwa Mazingira. Katika Kusimamia mazingira miradi ifuatayo imeandaliwa Tathimini Ndogo za Athari kwa Mazingira.
    - Mradi wa Uchenjuaji Dhahabu wa Selemani Juma Malale iliopo Mtinga
    - Mradi wa Uchenjuaji Dhahabu wa Hassan Athuman and Partner iliopo Mtinga.
    - Usimamizi wa Mazingira katika migodi ya uchimbaji dhahabu ya Katente, Msitu wa Hifadhi wa Ushirombo, Bulangwa, Kerezia na Ng'anzo.
- Usimamizi wa Kitalu cha Miti Bulama

### 3.1 KAZI ZILIZOFANYIKA

**Jedwali Na.11 - Uzoaji wa taka ngumu kwenye Vizimba**

| Na. | SHUGHULI | HALI YA UTEKELEZAJI | % UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Kusimamia Vikundi vya Usafi Kuondoa Taka tripu 400 ifikapo Juni 2021 katika Miji ya Ushirombo na Uyovu | Tripu za taka 40 zimeondolewa katika mji wa Ushirombo | 10 |
| 2. | Kukusanya tozo za usafi kiasi cha TSh 12,000,000/= ifikapo Juni 2021 | Kiasi cha Tsh 4,500,000/= zimekwisha kukusanywa | 37 |
| 3. | Kutunza, Kuuza na Kusambaza Miche ya Miti 30,000 ifikapo Juni 2021 | Miche ya Miti 400 imeuzwa kiasi cha Tsh 100,000/= imekusanywa. | 25 |

## 3.2 MAFANIKIO YA IDARA KIUJUMLA

Idara imefanikiwa kusimamia Mazingira katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za kibinadamu. Vilevile Idara imefanikiwa Kuondoa Taka katika Miji ya Ushirombo na Uyovu kwa wakati.

## 3.3 CHANGAMOTO

Changamoto zilizopo katika Idara ni kama ifuatavyo

- Upungufu wa Watumishi
- Ukosefu wa Vitendea kazi kama vile magari ya kuzolea taka etc
- Ufinyu wa bajeti

## 3.1.7 UTATUZI WA CHANGAMOTO.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Idara imeendelea kutatua changamoto zilizopo kwa kushirikiana na Idara nyingine, Sekta binafsi na Jamii katika kutekelezwa majukumu yake.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha.

## TAARIFA YA IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020

### 4.0 UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti;***

Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ni miongoni mwa Idara 12 na Idara 06 zilizo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Kiutawala.

### 4.1 Hali ya Utumishi

***Mhe. Mwenyekiti;***

Idara hii ina jumla ya Watumishi (Wataalam) Wanne (04) ambapo Watumishi 02 ni Wachumi, Watumishi 02 ni Watakwimu na hivyo kufanya upungufu wa Watumishi 03 ili kukamilisha ikama.

#### 4.1.2 Majukumu ya Idara

***Mhe. Mwenyekiti;***

Majukumu makuu ya Idara hii ni kama ifuatavyo:-

i. Kumshauri Mkurugenzi juu ya masuala ya maendeleo ya Kiuchumi ya Halmashauri.
ii. Kuratibu shughuli za maendeleo ya Halmashauri.
iii. Kuratibu na kusimamia utayarishaji wa Mipango ya kila mwaka ya Halmashauri na kufuatilia utekelezaji wake.
iv. Kuandaa na kuratibu shughuli za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Halmashuri kwa kila robo mwaka na kuziwasilisha kwenye kamati husika za Halmashuri, TAMISEMI na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.
v. Kuratibu maandalizi ya taarifa ya Utendaji kazi kwa Idara na Vitengo
vi. Kuandaa na kuratibu maandalizi ya taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya kila mwaka.
vii. Kuratibu maandalizi ya zoezi la upimaji utendaji wa Halmashuri (Assessment) kwa ajili ya kupata Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali Kuu.
viii. Kukusanya Takwimu muhimu za Kiuchumi na Kijamii.
ix. Kuratibu maandalizi ya Mpango na Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.
x. Kuandaa na kuratibu Mpango kazi (Action Plan) wa Halmashuri wa kila mwaka.

#### 4.1.3 Utendaji Kazi Julai, 2020 hadi Novemba, 2020

Miongoni mwa kazi zilizofanywa na Idara hii katika kipindi cha Julai- Septemba, 2020 ni:-

i. Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika ngazi ya Kata na Wilaya.
ii. Kuratibu na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na kuziwasilisha Mkoani na TAMISEMI.
iii. Kukusanya takwimu mbalimbali toka katika Mitaa, Kata, na Vijiji.
iv. Kuandaa taarifa ya Utendaji kazi na Utekelezaji wa Miradi kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2020/2021.
v. Kuratibu maandalizi ya taarifa ya Utendaji kazi kwa Idara na Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya.
vi. Kutengeza bakaa za Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo na kuingiza kwenye mfumo wa PlanRep.
vii. Kuandaa maandiko mbalimbali ya Miradi ya Maendeleo.
viii. Kuandaa Taarifa mbalimbali zinazohitajika kwa Wilaya na Mkoa Mfano Taarifa KUU, Taarifa za mwezi , Taarifa za CDR n.k
ix. Kuandaa nyaraka za maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 nakuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.
x. Kuandaa Mpango kazi wa Halmashauri kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

### 4.2 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto ambazo Halmashauri ya Wilaya inakumbana nazo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yake mbalimbali

i. Upandaji wa bei za ununuzi wa Saruji na Vifaa vingine vya ujenzi upatikanaji wake ni tatizo. Wazabuni wengi hutoa huduma wetu wamekuwa wakipandisha gharama mara kwa Mara.
ii. Changamoto ya upatikanaji wa Mafundi kutokana na kigezo cha Asilimia 10 ya gharama za vifaa hii imesababisha Miradi mingi kutokupata mafundi kwa wakati na kusababisha mchakato wa zabuni za mafundi kurudishwa zaidi ya mara tatu.
iii. Kuletwa kwa ramani na B.O.Q kutoka kwenye Wizara/Wafadhi zinazotoa fedha. Hali hii inapelekea Mradi kusuasua katika ukamilishaji. Mfano Miradi ya SWASH – Kwa shule za Msingi na WASH – Kwa upande wa Afya
iv. Baadhi ya Miradi kupewa fedha za utekelezaji mapema na maelekezo yake kuja kwa kuchelewa kutoka kwenye vyanzo vya Fedha hizo. Mfano Fedha za SWASH zilizotolewa Januari 2020 na maelekezo pamoja na miongozo

kutolewa mwezi Mei 2020.

v. Miradi mingi inayoanzishwa na wananchi kuchelewa kukamilika kutokana na wingi wa miradi na michango mbalimbali kwenye eneo husika.

vi. Ukosefu wa Fedha za Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo kuanzia ngazi ya Wilaya hadi ngazi ya vijiji na hii imesababisha Wataalam kutofika site kwa wakati muafaka na pindi wanapohitajika husuani idara ya Ujenzi.

## 4.3 MIKAKATI ILIYOWEKWA KWA AJILI YA KUTATUA CHANGAMOTO HIZI ILIKUHAKIKISHA MIRADI INAKAMILIKA KWA WAKATI

Zifuatazo ni baadhi ya Mikakati ambazo Halmashauri ya Wilaya imeweka kwa ajili ya kutatua/kukamiliana na changamoto hizo ilikuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati;

i. Halmashauri imeanzisha utaratibu wa kununua vifaa kwa pamoja ambapo imeanza kuagiza SARUJI za maeneo yote yenye utekelezaji kutoka Kiwanda cha Dangote ambapo bado kuna changamoto ya uzalishaji Kiwandani.

ii. Changamoto ya upatikanaji wa Mafundi kwa kigezo cha asilimia 10 ya gharama ya vifaa, Halmashauri imefanya jitihada kila wakati kwa kufanya mazungumzo “Negotiation” na Mafundi ya malipo yao kwa vigezo vilivyowekwa. Lengo ni mafundi hao waweze kufanya kazi kutegemeana na mpango kazi uliowekwa japokuwa mwitikio toka kwa mafundi bado ni mdogo sana gharama hiyo ya asilimia 10 inahitaji kupanda kulingana na hali ya maisha kwa sasa.

iii. Kuhusu changamoto yakuletewa Ramani na B.O.Q toka kwenye vyanzo vya fedha, Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikifanya mapitio ya michoro, Ramani, B.O.Q na kuwasilisha mapungufu yanayopatikana kwa mamalaka zinazotoa fedha hizo.

iv. Halmashauri ya Wilaya kuendelea kufanya mawasiliano na mamlaka zinazotoa fedha ilikupata Mwongozo wa matumizi moja kwa moja na kwa haraka.

v. Miradi viporo inayoanzishwa na nguvu za wananchi changamoto hii imewasilishwa OR-Tamisemi kipindi cha maandalizi ya Mipango na bajeti yam waka 2020/2021 japokuwa Miradi iliyopewa kipaumbele bado fedha yake haijaletwa.

vi. Suala la ukosefu wa fedha za ufuatiliaji, Halmashauri imewasilisha changamoto hii OR- Tamisemi ili mwongozo wa bajeti wa mwaka 2021/2022 uzingatie suala hili.

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YA ELIMU MSINGI KWA KIPINDI KUANZIA TAREHE 1 JULAI HADI 30 NOVEMBA 2020**

## 5.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Bukombe ni kati ya Halmashauri tano zilizopo katika Mkoa wa Geita. Idara ya Elimu Msingi kiutawala ina jumla ya Kata 17 na shule za msingi themanini na sita (86) zikiwepo shule za Serikali themanini (80) na shule za binafsi sita (06). Aidha, Halmashauri ina jumla ya wanafunzi 96,447 ikiwa ni wavulana 48,148 wasichana 48,229 Idara ya Elimu Msingi ina jumla ya walimu 1,041 wakiwemo me 548 na ke 493 Upungufu ni walimu 1,102

## 5.1 KAZI ZILIZOFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI - NOVEMBA, 2020.

Kwa kipindi cha Mwezi Julai – Novemba, 2020 kazi mbalimbali za kielimu zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Shule zilizopokea fedha za EP4R
ii. Ufuatiliaji na Usimamizi wa Mwalimu na Wananfunzi katika Shule zote 80 za Wilaya
iii. Usimamizi wa Zoezi la Mitihani wakumaliza Elimu ya Msingi kwa Watahiniwa 5,797 na mtihani wa upimaji Darasa la IV watahiniwa 14,118.

## 5.2 FEDHA ZA ELIMU BURE

Halmashauri ya Bukombe kwa shule za msingi imepokea jumla ya TZS 245,510,147,.58 ikiwa ni fedha ya elimu bila malipo. Kati ya hizo TZS 164,510,147.58 ni RUZUKU ya uendeshaji wa shule, TZS 64,000,000.00 posho ya madaraka ya walimu wakuu 80 na TZS 17,000,000.00 posho ya madaraka ya Maafisa Elimu Kata 17.

## 5.3 TAHADHARI YA COVID 19.

Shule zote 86 zilitembelewa kwa ajili ya kutoa Elimu kuhusu tahadhari ya ugonjwa wa Covid 19 na kuhamasisha walimu, wazazi na wageni wanaofika shuleni, kufuata maelekezo yote yaliyotolewa na wataalamu dhidi ya ugonjwa wa Covid 19

## 5.4 UJENZI WA VYUMBA VYA MADARSA – EP4R

Mwishoni mwa mwezi Juni 2019/2020 Halmashauri ilipokea Kiasi cha Tshs: 720,000,000.00 za EP4R awamu ya Nane (Lipa kutokana na matokeo) ziliingizwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo. Pesa hii iliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule, kwa maelekezo ya kujenga vyumba vya madarasa na vyoo.

Kamati Usimamizi (Ujenzi, Manunuzi, Mapokezi na Ufuatiliaji) ziliundwa na zinaendelea kusimamia shughuli za ujenzi kwa shule 08 ambazo ni S/M Ibamba, Kasozi, Namonge, Namalandula, Uyovu, Kabuhima, nampalahala na Bulega ambazo zilizopata fedha za EP4R.

Mpaka sasa Ujenzi wa miundombinu ya madarasa kwa shule zote 08 zilizoingiziwa fedha zinaendelea na utekelezaji.

## 5.5 UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VYOO - SWASH

Mwishoni mwa mwezi Januari, 2020 Halmashauri ilipokea Kiasi cha Tshs: **175,328,504.80** za SWASH kwa ajili ya ujenzi wa vyoo matundu 13 ziliingizwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. Pesa hii iliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule, kwa maelekezo ya kujenga vyoo ambayo yalitolewa Mwezi Mei, 2020 toka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Kamati Usimamizi (Ujenzi, Manunuzi, Mapokezi na Ufuatiliaji) ziliundwa na zinaendelea kusimamia shughuli za ujenzi kwa shule 07 ambazo ni S/M Bomani, Bulangwa, Nasiluluma, Isemabuna, Ituga, Kapela na Ikuzi ambazo zilizopata fedha za SWASH.

Mpaka sasa Ujenzi wa miundombinu ya vyoo hivyo kwa shule zote 07 zilizoingiziwa fedha zinaendelea na utekelezaji.

## 5.6 CHANGAMOTOZA IDARA

Katika Idara ya Elimu Msingi ina changamoto mbalimbali kama **ifuatavyo :-**

**Jedwali Na; 12**

| Aina ya changamoto | Mahitaji | Yaliyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Vyumba vya madarasa. | 2,144 | 822 | 1,322 |
| Matundu ya vyoo | 3,858 | 736 | 3,122 |
| Walimu | 2,143 | 1,041 | 1,102 |

## 5.7 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.

- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 208, matundu ya vyoo 194 na nyumba za walimu 16 vinaendelea na vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji
- Kuendelea kuomba walimu kutoka OR – TAMISEMI ili kukabiliana na upungufu unaoikabili Idara.

## JEDWALI NA; 13 - TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA

| NA | ENEO LA MRADI | HALI YA UTEKELEZAJI | TAREHE YA KUANZIA | TAREHE YA KUMALIZA | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA BAKIA | CHANGAMOTO / MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa vyumba 22 vya madarasa Shele ya Msingi Ibamba | 1).Ibamba shule ya msingi vyumba 04 na ofisi 02 viko hatua ya lenta.<br>(i). Kasongola vyumba 04 na Ofisi 01 hatua ya lenta.<br>(ii). Azimio sule ya msingi vyumba 03 vimeezekwa, vyumba 02 vinapandishwa kenchi.<br>(iii). Vyumba 02 hatua ya jamvi<br>(iv). Lyobahika vyumba 02 jamvi limekamilika 02 lenta na vyumba 03 uwekaji dari. | 20/11/2020 | 20/12/2020 | 440,000,000 | 44,000,000 | 396,000,000 | Wajumbe kutokuhudhuria vikao Jamii kujitolea nguvu kazi kwa kusua sua. |
| | | 2).Kabuhima vifaa kama vile Mbao, Top za Milango vimenunuliwa. | 23/10/2020 | 22/12/2020 | 40,000,000.00 | 4,576,830.00 | 35,423,670 | Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| 2 | Kasozi Shule ya Msingi Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa | Jengo linafungwa lenta. | 18/11/2020 | 18/12/2020 | 40,000,000.00 | 4,223,335.00 | 35,776,665 | Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa Shule ya Msungi Bulega. | Vifaa kama vile Mbao,Mabati ,Ceilling board vimenunuliwa | 15/11/2020 | 16/12/2020 | 40,000,000.00 | 8,760,000.00 | 36,240,000 | Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| 3 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa Shule ya Msungi Namonge | Vifaa kama vile Ceilling board, Gypsum,Rangi na Vigaevimenunuliwa | - | - | 40,000,000.00 | 3,944,260.00 | 36,055,740 | Fundi hajapatikana na Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| 4 | Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa Shule ya Msingi Nampalahala. | Ceilling board na PVC zimenunuliwa | 16/11/2020 | 16/12/2020 | 40,000,000.00 | 22,300,000.00 | 17,700,000, | Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| 5 | Ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa Shule ya Msingi Namalandula.. | Uezekaji pamoja na manunuzi ya vifaa vingine vya ujenzi unaendelea | 20/11/2020 | 20/12/2020 | 40,000,000.00 | 2,958,165.00 | 37,014,835, | Saruji haijaja kutoka kiwandani |
| 6 | Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa Shule ya Msingi Uyovu. | umwagaji jamvi pamoja na manunuzi ya vifaa vingine vya ujenziunaendelea | 29/11/2020 | 29/1292020 | 40,000,000.00 | 11,613,345.00 | 28,368,655 | Saruji haijaja kutoka kiwandani |

## JEDWALI NA; 14 - TAARIFA YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VYOO

| NA | ENEO LA MRADI | HALI YA UTEKELEZAJI | TAREHE YA KUANZIA | TAREHE YA KUMALIZA | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA BAKIA | CHANGAMOTO / MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa vyoo matundu 7 Shule ya Msingi Bulangwa | Mradi umekamilika | 06-12-20 | 31/7/2020 | 15,615,786.40 | 14,968,950 | 646,836.40 | hakuna |
| 2 | Ujenzi wa vyoo matundu 24 Shule ya Msingi Bomani. | jengo limeezekwa na kupakwa rangi | 15/06/2020 | 15/09/2020 | 33,911,786.40 | 32,890,720 | 1,021,066.40 | kasi ndogo ya wnajamiii kushiriki nguvu kazi |
| 3 | Ujenzi wa vyoo matundu 17 Shule ya Msingi Nasiluluma. | jego limeezekwa, upigaji lipu unaendelea. | 18/06/2020 | 19/09/2020 | 26,287,786.40 | 20,200,000 | 6,087,786.40 | kasi ndogo ya fundi katikaujenzi |
| 4 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 Shule ya Msingi Isemabuna. | jengo limeezekwa na kukupakwa rangi umaliziaji unaendelea. | 20/06/2020 | 30/11/2020 | 15,935,786.40 | 13,495,000 | 2,440,786.40 | umalliziaji unaendelea. |
| 5 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 Shule ya Msingi Ikizi. | maboma yamefungwa lenta maboma yanaendelea kujengwa. | 08-05-20 | 09-05-20 | 27,891,786.40 | 17,941,900 | 9,949,886.40 | umalliziaji unaendelea. |
| 6 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 Shule ya Msingi Kapela. | Mradi umekamilika | 21/06/2020 | 16/10/2020 | 27,793,786.40 | 22,688,000 | 5,105,786.40 | |
| 7 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 Shule ya Msingi Ituga. | jengo limeezekwa na kukupigwa lipu umaliziaji unaendelea. | 16/07/2020 | 16/10/2020 | 27,891,786.40 | 21,045,695 | 6,846,091.40 | umalliziaji unaendelea. |
| **JUMLA KUU** | | | | | **175,328,504.80** | **143,230,265.00** | | |

## JEDWALI NA; 15 -TAARIF YA UJENZI WA NYUMBA MBILI ZA WALIMU

| NA. | ENEO LA MRADI | HALI YA UTEKELEZAJI | TREHE YA KUANZA | TAREHE YA KUMALIZA | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA BAKIA | CHANGAMOTO /MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa nyumba moja ya mwalimu S/M Ibambilo | Mradi umekammilika | 8/05/2020 | 30/09/2020 | 25,000,000 | 23,600,000 | 1,600,000 | Fedha iliyobakia itatumika katika kukarabati Darasa |
| 2. | Ujenzi wa nyumba moja ya mwalimu S/M Nyamangwangala | Jengo Limeezekwa, ,Kupigwa Lipu na kuwekewa milango ya ndani na nje na umaliziaji unaendelea. | 3/05/2020 | 30/09/2020 | 25,000,000 | 12,536,000 | 12,464,000 | Fundi wa awali aliacha kazi na kuaijri fundi mwingine |

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha.

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YA ELIMU SEKONDARI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2020 – NOVEMBA, 2020

### 6.0 UTANGULIZI

Idara ya Elimu Sekondari ni miongoni mwa Idara **12** na vitengo **06** katika Halmashauri ya Bukombe. Idara hii inatoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya shule, usimamizi na uendeshaji wa Mitihani, sambamba na kusimamia na kuinua Taaluma katika shule zote za sekondari.

### 6.1 IKAMA YA WALIMU:

Idadi ya walimu wa sekondari katika wa Bukombe ni **525** ambapo kati yao Walimu wa Sayansi ni **85** na Walimu wa Sanaa ni **440** Halmashauri ina upungufu wa Walimu Sayansi na Hesabati na **135**. Aidha idara inaziada ya Walimu 144 wa masomo ya sanaa.

### 6.2 IDADI YA SHULE NA WANAFUNZI

Halmashauri ya BUKOMBE ina jumla ya Shule za Sekondari kumi na nane (18), kati ya Shule hizo, shule kumi na tano (15) ni za Serikali na Shule tatu (**03**) ni za Binafsi (zisizo za Serikali).

Halmashauri pia ina jumla ya Wanafunzi **13,879** wakiwemo Wavulana 7,322**.** na Wasichana **6,547** ikiwa wanafunzi **13,506** ni wa shule za serikali, wavulana wakiwa **7,062** na wasichana **6,444** Aidha wanafunzi **373** ni wa shule za binafsi, kati yao wavulana ni **270** na wasichana ni **103.**

### 6.3 UFUATILIAJI WA TAALUMA

Ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji umefanyika katika shule zote za sekondari kwa kipindi cha Miezi yote kuanzia Juali - Novemba 2020.

### 6.4 KURATIBU ELIMU YA JINSI YA KUJIKINGA NA CORONA.

Uratibu wa mafunzo juu ya elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa wa CORONA yalitolewa na wataalam wa Afya kwa shule zote na mafunzo ya awali yalishatolewa kwa walimu wa afya.

### 6.5 KURATIBU MITIHANI YA TAIFA KIDATO SITA 2020 NAMTIHANI WA TAIFA WA UPIMAJI KIDATO CHA PILI 2020.

Jumla ya watahiniwa **150** walisajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha sita 2020 katika Shule ya Sekondari Runzewe. Watahiniwa wa shule walikuwa **133** ambapo wote ni wavulana. Pia watahiniwa **17** walikuwa ni wa wakujitegemea, ambapo wavulana walikuwa **14** na wasichana ni **03**

Kwa upande wa kidato cha pili, jumla ya watahiniwa 3,672 walisajiliwa kufanya mtihani wa Taifa wa Upimaji kidato cha pili **2020**, ambapo kati yao **1,823** ni wavulana na **1849** ni wasichana.

Watahiniwa waliofanya Mtihani ni 3,390 ambapo Wavulani 1,676 na wasichana 1714 na wasiofanya Mtihani ni 282 Wavulana 147 na wasichana ni 135. Sababu kubwa iliyowafanya kwa baadhi ya watahiniwa kutokufanya mtihani ni Utoro.

## 6.6 MAPOKEZI YA FEDHA ZA ELIMU BILA MALIPO

Kuanzia Julai hadi Oktoba 2020, Jumla ya **Tshs. 164,000,112.00** zimepokelewa, ikiwa

- Fidia ya ada ni Tshs. **63,076,800.00**
- Chakula **Tshs. 37,536,000.00**
- Ruzuku ya uendeshaji **Tshs. 48,387,312.00**
- Posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule **Tshs. 15,000,000.00**

## 6.7 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA SITA 2020

### 6.7.1 SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE

Halmashauri ya BUKOMBE ina shule moja ya serikali yenye kidato cha tano na sita. Jumla ya watahinwa **133**, waliandikishwa kufanya mtihani wa kidato cha sita **2020**. Watahiniwa **133**, walifanya mtihani huo na mtahiniwa 01 hakuweza kufanya kwa sababu za ugonjwa.

### 6.7.2 MATOKEO YA MITIHANI

Matokeo ya Kidato cha Sita kwa Shule ya Runzewe nikama ifuatavyo ;

| | | |
|---|---|---|
| Division | I | 33 |
| Division | II | 71 |
| Division | III | 28 |
| Divison | IV | 00 |
| Division | 0 | 01 |

## 6.8 MAPOKEZI YA FEDHA ZA EP4R

Halmashauri ilipokea jumla ya Tsh 226,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa,Ujenzi wa Vyoo matundu 06, Ukamilishaji wa Bwalo na Bweni la Wananfunzi katika Shule ya Sekondari Bukombe.

Pia Halmashauri imepokea Kiasi cha Tshs. 67,700,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba vitatu vya madarasa na Matundu ya Vyoo 07 katika Shule ya Sekondari Businda.

Kamati za Usimamizi (Kamati ya Ujenzi, Kamati ya Manunuzi, Kamati ya Mapokezi na Kamati ya Ufutatiliaji) zimeundwa, Ujenzi/Ukamilishaji unaendelea na upo katika hatua mbalimbali na taratibu za manunuzi ya Vifaa kwa Kupitia wazabuni unaendelea kwa Shule zote

**6.9 PESA ZA MOTISHA**

Halmashauri ilipokea Tsh. **30,000,000.00** kwa ajili ya fedha za motisha kutoka mradi wa EP4R. Kiasi cha shilingi **15,000,000.00** kilitengwa kwa ajili ya kuimarisha IKAMA na kiasi cha shlingi **15,000,000.00** kilikuwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa taaluma na takwimu.

**6.10 PESA ZA UFUATILIAJI**

Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi **4,000,000.00** kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya EP4R ya ujenzi wa miradi ya ujenzi katika Sekondari za Businda na Bukombe kutoka mradi wa EP4R.

**6.11 CHANGAMOTO**

Idara ya Elimu Sekondari inachangamoto katika uhitaji wa Miundombinu mbalimbali kwamchanganuo ufuatao **;**

**JEDWALI NA ; 16**

| HALMASHAURI | 2019 | | |
|---|---|---|---|
| | MAHITAJI | VILIVYOPO | UPUNGUFU |
| MADARASA | 275 | 131 | 144 |
| VYOO | 445 | 231 | 214 |
| MAABARA | 45 | 44 | 1 |
| NYUMBA | 521 | 64 | 457 |

6.12 **MIKAKATI YAKUTATUA CHANGAMOTO**

- Halmashauri ya Wilaya inaendelea kuhamasisha wananchi katika kukamilisha Miundo mbinu hiyo.
- Halmashauri inaendelea kutenga Bajeti kila mwaka wa Fedha kwa ajili ya kukamilisha miundo mbinu hiyo
- Halmashauri imeomba fedha Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu.

*Mhe. Mwenyekiti*

Nawasilisha.

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YA AFYA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020.**

## 7.0 UTANGULIZI.

*Mhe. Mwenyekiti*

Idara ya afya Bukombe ina jumla ya vituo 14 vya kutolea huduma za afya ;Hospitali ya Wilaya 01,Vituo vya afya 04 na zahanati 09 ambavyo vinamilikiwa na Serikali. Pia kuna jumla ya vituo vya tiba 07 ; Hospitali 01, Kituo cha Afya 01 na Zahanati 05 ambavyo ni vya binafsi;

Timu ya Uendeshaji Wa Shughuli Za Afya (CHMT) imekuwa ikisimamia utekelezaji wa wa shughuli zote za afya ,maendeleo ya jamii,jinsia ,wazee na watoto.

## 7.1 MAJUKUMU YA IDARA YA AFYA

*Mhe. Mwenyekiti*

### 7.1.1 **Ofisi ya Mganga Mkuu**

Usimamizi wa shughuli za Afya kinga, kufanya usimamizi shirikishi, usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kupanga na kutatua changamoto mbalimbali za Idara, kutoa huduma kwa watu wenye mahitaji maalum na kutekeleza mipango mkakati katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Halmashauri

### 7.1.2 **Vituo vya Tiba na Zahanati**

Kutoa huduma ya mama na mtoto ikiwepo kujifungua kama hospital, pia wagonjwa wa nje na wagonjwa wa ndani, uzazi wa mpango, upasuaji, chanjo, huduma za VVU na Elimu ya Afya kwa ujumla.

## 7.2 IDADI YA WATUMISHI KWA VITUO.

Idara ya afya Bukombe ina jumla ya watumishi 322 kwa ujumla katika vituo vyote vya kutolea huduma na inaupungufu wa watumishi 108 Kulingana na ikama.

Jedwali Na; 17 - Watumishi hao wamegawanya katika mchanganuo ufuatao;

| **Na.** | **Jina La Kituo** | **Idadi Ya Watumishi** |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mganga Mkuu (W) | 17 |
| 2 | Hospitali ya Wilaya | 154 |
| 3 | Kituo cha Afya Uyovu | 53 |
| 4 | Kituo cha Afya Ushirombo | 42 |
| 5 | Kituo cha Afya Bulega | 14 |
| 6 | Kituo cha Afya Namonge | 6 |
| 7 | Zahanati ya Bukombe | 6 |
| 8 | Zahanati ya Iyogelo | 6 |

| Na. | Jina La Kituo | Idadi Ya Watumishi |
|---|---|---|
| 9 | Zahanati ya Bugelenga | 7 |
| 10 | Zahanati ya Bugando | 4 |
| 11 | Zahanati ya Ikuzi | 7 |
| 12 | Zahanati ya Miyenze | 3 |
| 13 | Zahahanti ya Msasani | 3 |
| 14 | Zahahanti ya Bulangwa | 6 |
| 15 | Zahanati ya Businda | 4 |
| **JUMLA** | | **332** |

Hata hivyo katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Novemba 2020 mtumishi mmoja alifariki (Sharifa S.Milele), watumishi wawili walihamia katika wilaya yetu Days Shem ambaye ni Muuguzi na Wibert Musiba ambaye ni Daktari .

Pia watumishi wawili walibadilishiwa vituo vya kazi, Ghati Mary Marwa (Muuguzi) kutoka Ushirombo kwenda Hospitali ya Wilaya na Sagenge Maningu (Tabibu) kutoka Ushirombo kwenda Zahanati ya Bukombe.

## 7.3 MIUNDO MBINU

### 7.3.1 FEDHA ZA WASH.

*Mhe. Mwenyekiti*

Mwishoni mwa mwezi Januari, 2020 Halmashauri ilipokea kiasi cha Tsh. 220,000,000.00 ikiwa ni Fedha za WASH kwa ajili ya usimamizi, ujenzi wa vyoo, ukarabati wa vyoo na kurekebisha miundo mbinu ya maji katika Vituo vya Tiba 10. Pesa hii iliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za Vituo vya kutolea huduma za Afya, kwa maelezo yalitolewa mwezi Mei, 2020 toka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Jedwali Na; 18 -Mchanganuo wa matumizi na utekelezaji kwa kila kituo umeambatanishwa.

| Na | Eneo La Utekelezaji | Fedha Tolewa | Fedha Tumika | Fedha Bakia | Hatua Ya Mradi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Wilaya | 36,000,000.00 | 24,000,000.00 | 12,000,000.00 | Hatua za Ujenzi unaendelea Choo cha Matundu 02 kipo hatua ya Kumalizia |
| | | | | | Ukarabati wa vyoo vya wagonjwa wa ndani unaendelea |
| | | | | | Ujenzi wa matanki 03 unaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji unaendelea |
| 2 | Kituo cha Afya Ushirombo | 40,000,000.00 | 24,120,000.00 | 15,880,000.00 | choo cha watumishi kipo katika hatua ya kupakwa rangi |
| | | | | | choo cha wagonjwa wa OPD vimeshapigwa lipu na rangi vimepakwa |
| | | | | | Ujenzi wa tanki 01 unaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji unaendelea |
| 3 | Kituo cha Afya Uyovu | 45,500,000.00 | 16,827,600.00 | 28,672,400.00 | Ukarabati kwa jengo la ufuaji umefanyika |
| | | | | | Shimo la choo limechimbwa na boma lipo hatua ya kumwaga jamvi katika msingi |
| 4 | Kituo cha Afya Bulega | 5,000,000.00 | 3,000,000.00 | | Fedha hii imepokelewa tarehe 02/11/2020 imetumika kuchimba kisima cha maji wako katika hatua ya umaliziaji |
| 5 | Zahanati ya Ikuzi | 23,000,000.00 | 23,000,000.00 | | Choo cha Watumishi matundu 02 kimepigwa lipu na shimo limeshafunikwa |
| | | | | | Vifaa vya maji vimenunuliwa tayari na kusimika miundo mbinu ya maji kazi imeanza |
| 6 | Zahanati ya Bukombe | 11,000,000.00 | 10,921,600.00 | | Boma la vyoo vya watumishi limepauliwa |

| Na | Eneo La Utekelezaji | Fedha Tolewa | Fedha Tumika | Fedha Bakia | Hatua Ya Mradi |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Zahanati ya Bugelenga | 15,000,000.00 | 12,600,000.00 | | Boma la vyoo vya watumishi limekamilika na shimo la choo la kwanza limechimbwa bado la pili linajengwa |
| | | | | | Vifaaa vya maji vimenunuliwa tayari na ujenzi umeanza |
| 8 | Zahanati ya Iyogelo | 18,500,000.00 | 9,903,300.00 | | Choo cha wafanyakazi kipo hatua ya upauaji, Mashimo yanajengelewa , |
| | | | | | Vifaa vya maji vimeshanunuliwa tayari |
| 9 | Zahanati ya Bugando | 13,000,000.00 | - | | Fedha hii imepokelewa tarehe 02/11/2020 na taratibu za manunuzi mbalimbali ya vifaa vya ujenzi unaendelea ambapo kokoto, mawe, mchanga, tofali, cementi, na vifaa vya maji vimepelekwa tayari kituoni |
| 10 | Zahanati ya Miyenze | 13,000,000.00 | - | | Fedha hii ilipokelewa tarehe 2/11/2020 na taratibu za manunuzi zinaendelea pamoja na kupata mafundi. |
| **JUMLA** | | **220,000,000.00** | **124,372,500.00** | **56,552,400.00** | |

### 7.3.2 UJENZI WA MIUNDOMBINU MINGINE

#### i. Jedwali Na; 19 - Ujenzi wa kituo cha Afya Namonge

| Hali ya utekelezaji | Fedha pokelewa | Fedha tumika | Changamoto |
|---|---|---|---|
| Jengo la OPD | 200,000,000 | 187,795,340 | Uchangiaji wa wananchi ni mgumu – uongozi wa kijiji kushindwa kusimamia |
| Mama na mtoto | Nguvu kazi za wananchi 4,370,000 | 4,370,000 | |
| Vyoo vimekamilika | | | |
| Jengo la Maabara limekamilika | | | |

#### ii. Jedwali Na; 20 -Taarifa za uanzishwaji wa duka la duka la dawa (Hospitali ya Wilaya)

| **Hali ya utekelezaji** | **Tarehe ya kuanza** | **Tarehe ya kumaliza** | **Fedha pokelewa** | **Fedha tumika** | **Changamoto/ maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| Duka Limekamilika | 18/7/2019 | 31/5/2020 | 23,129,900 | 23,129,900 | Usajili wa duka |

#### iii. Jedwali Na; 21 - Kituo cha Afya Uyovu

| **Hali ya utekelezaji** | **Tarehe ya kuanza** | **Tarehe ya kumaliza** | **Fedha pokelewa** | **Fedha tumika** | **Changamoto/maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| Liko katika hatua ya kupiga ripu na gypsum board | Mei, 2020 | - | 15,000,000 | 15,000,000 | Hatua ya pili ya umaliziaji – tunasubiri fedha za RBF |

### 7.4 UPATIKANAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA

Idara ya Afya Bukombe ina upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na vifaa vya maabara. Hali hii imesababishwa na Serikali kutotuma fedha ya ruzuku kuu yaani( Receipt in kind, MSD) ,fedha hizi serikali huingizwa moja kwa moja MSD kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa ruzuku kuu ya serikali (MSD Receipt in kind) fedha hazijatumwa hadi sasa.

Kama jedwali linavyo onesha.

JEDWALI NA; 21 - HALI YA DAWA NA VIFAA TIBA MWAKA 2020/21.

| **CHANZO CHA FEDHA** | **BAJETI KWA MWAKA** | **ROBO YA I-(JULAI-SEPTEMBA)** | **FEDHA TOLEWA** | **MAONI/MAELEZO** |
|---|---|---|---|---|
| HSBF | 207,039,627.95 | 103,519,813.05 | HAKUNA | Serikali haijaleta fedha tangu mwaka huu wa fedha uanze |
| RBF | 166,611,703.00 | 83,305,851.50 | HAKUNA | |
| MSD | 571,735,790.00 | 285,867,895.00 | HAKUNA | |
| JUMLA | 945,387,120.95 | 472,693,559.55 | HAKUNA | |

*Mhe. Mwenyekiti*

Upungufu huu unasababishwa na Hospitali kutoweza kununua dawa au kukopa dawa toka kwa mshitiri au bohari kuu ya dawa (MSD) changamoto hii ni kwa sababu Hospitali inadaiwa na MSD Kiasi cha Tsh.68,669,975.71 na Tsh. Milioni 22.3 na mshitiri.

Madeni haya mpaka sasa hayajalipwa, hivyo Idara inajitahidi kutatua changamoto hiyo kwa kuhamamsisha makusanyo ya vyanzo vya ndani kama vile NHF, Fedha za papo kwa papo na Ichf ingawa mapato yameshuka sana kutokana na kutokuwepo kwa dawa na vifaa tiba na wateja kupungua.

Mpaka sasa vituo karibu vyote vya kutolea huduma za afya havina dawa na vifaa tiba pamoja na vipimo vya maabara kama vile vipimo vya kupima mimba, mkojo, choo kubwa na full Blood picture havifanyiki kwa sababu vitendanishi vimeisha na hatuwezi kuvinunua MSD kwa sababu hakuna fedha.

**7.5 CHANGAMOTO**

i. Fedha za RBF na HSBF kuchelewa kuja hivyo shughuli nyingi kutotekelezwa kwa wakati

ii. Uelewa mdogo kwa jamii juu ya umuhimu wa akina mama wajawazito kuwahi kuanza kiliniki mapema na kupelekea kushindwa kukamilisha mahudhurio yote 4 au zaidi na kutopata huduma zote anazopaswa kupata wakati wa kipindi chote cha ujauzito.

iii. Changamoto ya akina mama kujifungulia nyumbani bado ipo japo sio kwa wingi.

iv. Ushirikiano wa wanaume katika uzazi wa mpango uko chini sana.

v. Vituo vya kutolea huduma za Afya havitoshi kwani wananchi wengi wanaishi mbali na huduma nma huuduma za Afya.

**7.2 MIKAKATI INAYOWEZA KUTATUA CHANGAMOTO**

i. Kuja kwa fedha kwa wakati ili shughuli hasa zinazohitajika fedha kufanyika kwa wakati.

ii. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya faida ya huduma zinazotolewa wakati wa kiliniki za wajawazito wanapowahi kuanza kiliniki zao na matatizo ambayo yanaweza kutokea wakati ambapo mama mjamzito amekosa baadhi ya huduma kutokana na kuchelewa kuanza kiliniki.

iii. Kuktoa elimu kwa wananchi juu ya hatari ya kujifungulia nyumbani na matatizo ambayo hayawezi kutatuliwa yakitokea wakati anapojifunguliwa nyumbani, pia elimu juu ya usalama wa akina mama wajawazito wanapo jifungulia katika vituo vya kutolea huduma za Afya.

iv. Kukendelea kuhamasisha wanaume katika mikutano ya hadhara kupitia kamati za vituo kushiriki katika uzazi wa mango.
v. Kuhamasisha wananchi katika vijiji ambavyo havina vituo vya kutolea huduma za Afya kuanzisha ujenziw a zahanati na vituo vya Afya katika kata.
vi. Kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa CHF iliyoboreshwa.

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI, 2020 HADI TAREHE NOVEMBA, 2020**

## 8.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti*

Idadi kubwa ya Wakazi wa Wilaya ya Bukombe wanajihusishwa na kilimo cha Mazao ya Chakula na Biashara kama Mpunga, Viazi, Mihogo, Tumbaku na Mtama

## 8.1 IDADI YA WATUMISHI NA MAHITAJI WA IDARA YA KILIMO.

Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika ina jumla ya vitengo 04 ambavyo ni:-

i. Utawala
ii. Ushauri na Ugani
iii. Hifadhi ya Mimea
iv. Takwimu za Kilimo

Idara ina jumla ya watumishi 27 kati yao 3 wapo Ofisi kuu, Watumishi 16 wapo ngazi ya Kata na Watumishi 8 wapo ngazi ya kijiji

### 8.1.1 JEDWALI NA; 22 – MALENGO YA KILIMO MSIMU WA KILIMO 2020/2021

| ZAO | MALENGO | |
|---|---|---|
| | **ENEO (Ha)** | **MATARAJIO YA MAVUNO (Tani)** |
| Mahindi | 36,657 | 91,643 |
| Mpunga | 19,345 | 58,035 |
| Mtama | 1,932 | 2,318 |
| Uwele | 362 | 362 |
| Ulezi | 190 | 171 |
| **Mazao ya nafaka- Jumla** | **58,486** | **152,529** |
| Muhogo | 18,465 | 44,304 (Makopa) |
| Viazi Vitamu | 18,306 | 109,836 |
| **Mazao ya mizizi- Jumla** | **36,771** | **154,140** |
| Kunde | 2,576 | 1,803 |
| Maharage | 11,122 | 8,898 |
| Karanga | 13,693 | 12,324 |
| Njugumawe | 179 | 143 |
| Choroko | 55 | 39 |
| Mbaazi | 12 | 12 |
| **Mazao ya mikunde- Jumla** | **27,637** | **23,219** |
| Migomba ya Ndizi mbichi | 8 | 32 |
| Migomba ya Ndizi mbivu | 22 | 88 |
| **Mazao ya ndizi-Jumla** | **30** | **120** |
| Tumbaku | 693 | 1,040 |
| Pamba | 17,001 | 17,001 |
| Alizeti | 2,210 | 1,768 |
| **Mazao ya asili ya biashara-Jumla** | **19,904** | **19,809** |

**8.2 IDADI YA MASOKO**.

*Mhe. Mwenyekiti*

Halmashauri ina masoko madogo 17 na makubwa 06 ya mazao ya Kilimo ambayo yapo katika Kata ya Namonge (Namonge), Kata ya Uyovu (Ibamba na Lyobahika), Kata ya Runzewe Mashariki (Msonga), Kata ya Bukombe (Bukombe) na Kata ya Ushirombo (Ushirombo)

**8.3 IDADI YA MAGHALA.**

*Mhe. Mwenyekiti*

Kuna jumla ya maghala 6 ya UMMA yanayo tumika kuhifadhi mazao ambayo yapo katika Kata ya Ng'anzo - 01, Kata ya Bugelenga - 01, Kata ya Namonge -01 na Kata ya Bukombe – 02. Aidha kuna jumla ya maghala ya Watu binafsi yapatayo 23.

**8.4 UZALISHAJI WA MBEGU DARAJA LA KUAZIMIA.**

Katika Halmashauri kuna wazalishaji wawili wa mbegu za daraja la kuazimia kwa zao la Muhogo ambao ni Ndugu Bundala Maziku Mlalu wa Kata ya Namonge na ndugu Mdabulo paul wa Kata ya Runzewe Mashariki

**8.5 SOKO LA MAZAO.**

**8.5.1 BEI ZA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA.**

Wanunuzi wa mazao ya chakula ni wafanyabiashara na walaji, na soko linapatikana Wilayani Bukombe kwa wauzaji mmoja mmoja katika maeneo mbalimbali (Masokoni na magulioni).

**MWENENDO WA BEI YA MAZAO SOKONI KWA MWEZI OCTOBA 2020**

Vyakula katika masoko yetu bado vinapatikana kwa bei ya nafuu hasa kwa mazao ya nafaka kama mahindi na mihogo ukilinganisha na kipindi kama hiki msimu uliopita kama ilivyo oneshwa kwenye Jedwali hapo chini.

**Jedwali Na; 23 - MWENENDO WA BEI YA MAZAO**

| Na | Zao | Kipimo | Bei ya mazao (Tshs) Julai, 2019 |
|---|---|---:|---:|
| 1. | Mahindi | Debe | 10,000-12,000 |
| 2. | Mtama/Uwele | Kilo 1 | 1,000 |
| 3. | Mpunga | Debe | 9,000 |
| 4. | Mchele | Kilo 1 | 1,000- 1,200 |
| 5. | Makopa | Kilo 10 | 7,000 - 8,000 |
| 6. | Viazi Vikavu (Viazi Vitamu) | Kilo10 | 4,000 - 5,000 |
| 7. | Muhogo Mbichi | Fungu/Kilo | 1,000 |
| 8. | Viazi Vibichi (Viazi Vitamu) | Fungu/Kilo | 500 |
| 9. | Viazi Mviringo | Kilo 1 | 1,000 |

| Na | Zao | Kipimo | Bei ya mazao (Tshs) Julai, 2019 |
|---|---|---|---|
| 10. | Ndizi Kupika | Kilo | 1,000 |
| 11. | Ngano (Unga) | Kilo 1 | 1,200 |
| 12. | Sukari | Kilo 1 | 2,800 |
| 14. | Magimbi | Fungu | 500 - 2,000 |
| 15. | Maharage | Kilo 1 | 2,000 -2,500 |
| 16. | Njugu Mawe | Kilo 1 | 2,000 |
| 17. | Kunde | Kilo 1 | 1,000 |
| 18. | Njegere | Kilo 1 | 1,800 - 2,000 |
| 19. | Soya | Kilo 1 | 1,500 |
| 20. | Tikiti Maji | Kilo 1 - 5 | 500 - 2,000 |
| 21. | Nyanya | Ndoo | 15,000 - 18,000 |
| 22. | Ulezi | Kilo 1 | 1,500 |
| 23. | Kabichi | Kilo | 500 - 1000 |
| 24. | Unga wa Sembe | Kilo 1 | 1,200 - 1,500 |
| 25. | Ngano | Kilo 1 | 1,000 – 1,500 |

**Jedwali Na; 24 - Mazao ya Biashara.**

| Na | Zao | Kipimo | Bei ya Chini (Tsh) | Bei ya Juu (Tsh) | Bei ya wastani |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Pamba | Kilo | 810 | 900 | 855 |
| **2** | Tumbaku | Kilo | 3450 | | 3450 |
| **3** | Alizeti | Kilo | 560 | 580 | 570 |

### 8.5.2 Mahitaji ya pembejeo

Hali ya Uhitaji wa pembejeo kwa Wakulima wa Wilaya ya Bukombe nikama ifuatavyo;

**Jedwali Na; 25 – Mahitaji ya embejeo**

| S/N | Aina ya Pembejeo | Mahitaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1 | Mbolea za viwandani | 93.4 |
| 2 | Mbegu za mahindi | 916,425 |
| 3 | Mbegu ya Mtama | 9,660 |
| 4 | Mbegu ya Alizeti | 11 |
| 5 | Mbegu ya pamba | 180 |
| 6 | Viuadudu | Eka paka 170,010 |
| 7 | Vifaa vingine (mabomba ya solo,52, keni za kumwagilia maji 100 | |

## 8.6 HALI YA CHAKULA

*Mhe. Mwenyekiti*

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa malengo ni jumla ya Tani 130,746 za nafaka zilizozalishwa kutoka eneo la Hekta 71,716, Tani 47,373 za mazao makavu ya mizizi kutoka eneo la Hekta 51,720 za eneo lililolimwa na Tani 30,976 za mikunde zilizozalishwa kutoka Eneo la Hekta 28,935 zilizolimwa.

Kutokana na Wilaya ya Bukombe kuwa na jumla ya wakazi wapatao 301,403 ambapo mahitaji ya chakula ni Tani 77,261 za nafaka/mazao ya mizizi na Tani 29,716 za mikunde, tathmini hii inaifanya Wilaya kujitosheleza kwa chakula kwa mwaka mzima na ziada ya jumla ya Tani 96,858 za nafaka na mazao ya mizizi pamoja na Tani 1,260 za mikunde.

**FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA KILIMO.**

Fursa za uwekezaji zilizopo ni usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao mbalimbali na uzalishaji wa mazao ya biashara.

## 8.7 KAZI ZILIZOFANYIKA KUANZIA JULAI HADI NOVEMBA 2020

***Mhe. Mwenyekiti***

Pia Idara kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2020 imetekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuendelea kuhamasisha wakulima juu ya kanuni bora za uhifadhi wa chakula jumla ya kaya Kata 17 zilihamasishwa.
ii. Kuendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa malengo ya kilimo msimu 2020/2021 kwa mazao yote.
iii. Kusimamia udhibiti wa afya ya mimea na visumbufu vya mimea
iv. Kusimamia na kufuatilia soko la pamba hadi sasa jumla ya kilogramu 1,046,000 yenye thamani ya Tsh. 747,260,000 zilipimwa, kulipiwa na kusafirishwa.
v. Kundaa na kushiriki maonyesho ya nane nane 2020 yaliyofanyikia Nyamuhongolo Jijini Mwanza na kushika nafasi ya kwanza kwa kundi la wasindikaji.
vi. Kusimamia na kufuatilia soko la Tumbaku hadi sasa jumla ya kilogramu 307,357.97 yenye thamani ya Tsh. 1,078,512,251 zilipimwa, kulipiwa na kusafirishwa.
vii. Kufanya mikutano na vikao katika SACCOS 01 kuwapa elimu viongozi na wanachama kuhusiana na uendeshaji wa shughuli za SACCOS kuendana na sheria na Kanuni mpya za SACCOS na faida za kuwa mwana SACCOS ukilinganisha na Taasisi nyingine za fedha. SACCOS ambazo mikutano na vikao vilifanyika ni Wanawake SACCOS, Kndebona SACCOS
viii. Kusimamia mapokezi ya mbegu za pamba, ambapo jumla kuu ya tani pokelewa ni tani 180 katika AMCOS 47 za pamba

## 8.8 VYAMA VYA USHIRIKA.

**MUHTASARI WA VYAMA VYA USHIRIKA.**

Kitengo cha Ushirika kinasimamia jumla ya vyama vya Ushirika 107 ambapo vyama hai ni 69 na vyama sinzia ni 38 vilivyo katika mgawanyo ufuatao:

**JEDWALI NA; 26 – VYAMA VYA USHIRIKA**

| VYAMA | HAI | SINZIA |
|---|---|---|
| **AMCOS** | 51 | 4 |
| **SACCOS** | 6 | 16 |
| **MADINI** | **9** | **10** |
| **MIFUGO** | **2** | **4** |
| **VINGINEVYO** | **1** | **4** |
| **JUMLA** | **69** | **39** |

**8.9 CHANGAMOTO ZA KIUTENDAJI ZINAZOIKABILI OFISI.**

i. Mabadiliko ya tabia ya nchi (Hali ya hewa) yanayopelekea kuwa na mvua zisizotabirika na mlipuko wa magonjwa na wadudu katika mazao.
ii. Upungufu mkubwa wa wataalamu wa Kilimo kwenye ngazi ya kijiji.
iii. Uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Kilimo hususani ukarabati wa skimu ya umwagiliaji iliyopo Kijiji cha Nampangwe na Bugelenga
iv. Upungufu wa pembejeo za kilimo hasa mbegu bora ,mbolea na viuatilifu na hata vikipatikana bei yake ni kubwa

**8.10 UTATUZI WA CHANGAMOTO**.

i. Halmashauri kupitia Idara ya kilimo inaendelea kutoa elimu ya mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na kuwahimiza wakulima kulima mazao ya muda mfupi na yanayovumilia ukame na magonjwa
ii. Halmashauri inaendela kuomba vibali vya ajira ili kujaza nafasi zilizo wazi.
iii. Halmashauri kwa kushirikiana na Tume ya umwagiliaji imeandaa andiko kwa ajili ya kupata fedha za ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na ununuzi wa matrekta.
iv. Kuwaunganisha wakulima na wadau wa Kilimo ili kutatua changamoto za mashamba darasa na mashamba ya mfano Kushirikiana na wadau waliopo kama watafiti (TARI),CAPAFO,Meru Agro,YARA nk

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha;

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2020 – NOVEMBA, 2020**

## 9.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti*

Idara imeendelea kujishughulisha na uendelezaji wa mifugo na uvuvi ndani ya Halmashauri katika kipindi husika. Aidha miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na:-

i. Kutoa ushauri juu ya ufugaji bora, kinga na ufugaji wenye tija kwa wafugaji wote ndani ya Halmashauri ya BUKOMBE.
ii. Kutoa huduma za kuhasi na kutibu magonjwa mbalimbali.
iii. Kusimamia shughuli mbalimbali zinazofanyika machinjioni kama kusimama uchunaji, ukaguzi wanyama pamoja na kukusanya ushuru wa halmashauri utokanao na ng'ombe, mbuzi na kondoo waliochinjwa machinjioni hapo.
iv. Kukagua afya ya mifugo inayoingia mnadani kusimamia mauzo na kutoa vibali vya mifugo inayonunuliwa na kusafirishwa kutoka kwenye minada husika.

## 9.1 Watumishi:

**(a) Idara inajumla ya watumishi 13 kwa mgawanyo ufuatao**:-

i. Afisa Mifugo 3
ii. Afisa Uvuvi 0
iii. Afisa Mifugo wasaidizi 10

**(b) Upungufu**

Maafisa mifugo wasaidizi 10
Maafisa uvuvi 3

## 9.2 Sekta ya Mifugo

**Jedwali Na; 27 -Idadi ya Mifugo:**

| *Aina* | **Kienyeji** |
|---|---|
| Ng'ombe | 130,750 |
| Mbuzi | 93,400 |
| Kondoo | 21,500 |
| Kuku | 314,600 |
| Bata | 2,720 |
| Nguruwe | 7,631 |
| Punda | 1,770 |
| Mbwa | 1,500 |
| Paka | 280 |

## 9.3 JEDWALI NA; 28 -MIUNDOMBINU YA HUDUMA ZA MIFUGO ILIYOPO

| S/N | MIUNDOMBINU | IDADI | MAHALI ILIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | Minada ya mifugo | 2 | Busonzo na Bukombe |
| 2 | Mabanio | 4 | Namonge, Msonga, Ikuzi na Bugelenga |
| 3 | Mabirika ya kunyweshea mifugo | 2 | Ituga na Bukombe |
| 4 | Machinjio | 4 | Mwalo, Uyovu, Msinila na Katente |
| 5 | Visima kirefu | 2 | Mwalo na Katente |
| 6 | Majosho | 5 | Musasa, Bugando, Bukombe, Ituga na Msonga |
| 7 | Malambo | 4 | Bukombe, Bugando, Ituga na Iyogelo |

## 9.4 Shughuli za minada

- Jumla ya ng'ombe 2,703 wamepigwa chapa ili kuwatambulisha kuwa ni mifugo iliyopo wilayani Bukombe
- Matibabu na ushauri juu ya mifugo inayoumwa.

## 9.5 Huduma zilizotolewa kwa Mifugo

- ***Kuhasi***: jumla ya ng'ombe **98** na nguruwe **61** wamehasiwa.
- ***Kukata meno***: jumla ya nguruwe 81 wamekatwa meno.
- ***Uogeshaji*****:** jumla ya ng'ombe 6781 mbuzi 218, kondoo 69 na mbwa 39 wameogeshwa.

## 9.6 Changamoto za Idara:

i) Uchache wa maafisa ugani wa mifugo wa kata na vijiji.
ii) Uchache na uchakavu wa vitendea kazi.
iii) Uchache wa usafiri kwa maafisa ugani
iv) Ukosefu wa maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo na kupelekea migogoro vaina ya wakulima na wafugaji.

## 9.7 Mapendekezo;

I. Kupata wataalam wa mifugo ili kurahisisha namna ya kuwafikia wafugaji katika maeneo yote
II. Kutenga fedha kwenye bajeti kuu kwa ajili ya huduma za mifugo na kuajiri wataalamu
III. Kuendelea kuomba vibali vya kumegewa maeneo ya malisho kutoka kwenye mapori yaliyopo.

**9.8 Kitengo cha Uvuvi**

Wilaya ina jumla ya mabwawa 20 ambayo yana samaki aina ya sato na kambale yanayomilikiwa na watu binafsi.

**9.9 Changamoto zilizopo**

i. Ukosefu wa wataalamu wa uvuvi katika halmashauri
ii. Ukosefu wa vitendea kazi hasa vya usafiri

**9.10 Mapendekezo**

i. Kupata wataalamu wa uvuvi ili kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za uvuvi
ii. Kuwepo kwa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri ilikufanikisha shughuli za kiutendaji.

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YA ARDHI, MIPANGO MIJI NA MALIASILI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2020 – NOVEMBA, 2020**

## 10.0 UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti;***

Idara ya Ardhi na Maliasili ina Vitengo sita ambavyo ni Ardhi Usimamizi, Mipango Miji, Upimaji na Ramani, Uthamini, Misitu na Wanyapori.

Malengo Makuu ya Idara ya Ardhi na Maliasili kwa mwaka 2020/2021 ni manne kama yafuatayo:-

(a) Usimamizi wa shughuli za ukuaji wa Mji kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na uendelezaji wake.
(b) Kukusanya maduhuli ya Serikali
(c) Kuimarisha usimamizi wa Maliasili na Mazingira
(d) Kutatua migogoro ya ardhi
(e) Usimamizi wa sheria kwa masuala yote yanayohusu sheria, kanuni na taratibu za upimaji, mipango mji na ardhi.

## 10.1 TASWIRA YA WATUMISHI.

Idara ya Mipangomiji, Ardhi na Maliasili ina jumla ya watumishi 06 lakini kwa mujibu wa ikama, Sekta hii inahitaji watumishi 38 na hivyo ina upungufu wa Watumishi 32

**Jedwali Na. 29 -** Taswira ya Watumishi ( staff disposition)

| NA. | KITENGO | KADA YA WATUMISHI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mipangomiji | Afisa Mipangomiji | 0 | 2 |
| 2 | Upimaji | (i) Wapima ardhi | 1 | 2 |
| | | (ii) Fundi Sanifu upimaji | 0 | 2 |
| | | (iii)Wasanifu Ramani | 0 | 2 |
| | | (iv) Field Asst. | 1 | 4 |
| 3 | Maliasili | (i) Afisa Maliasili | 1 | 0 |
| | | (ii)Afisa Misitu Msaidizi | 1 | 5 |
| | | (iii) Afisa Nyuki Msaidiizi | 0 | 4 |
| 4 | Uthamini | (i) Wathamini | 0 | 2 |
| | | (ii) Wathamini wasaidizi | 0 | 3 |
| 5 | Ardhi | Afisa Ardhi Mkuu | 1 | 1 |
| | | Afisa Ardhi Mteule | 0 | 1 |
| | | Afisa Ardhi I | 0 | 1 |
| | | Afisa Ardhi W/Mwandamizi | 1 | 2 |
| | | Afisa Ardhi Wasaidizi | 0 | 3 |
| | | Mpiga chapa wa Kumbukumbu | 0 | 1 |
| | | Mtunza Kumb. | 0 | 1 |
| | | Wahudumu | 0 | 2 |
| **JUMLA KUU** | | | **6** | **32** |

## 10.2 KITENGO CHA MIPANGO MIJI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020, lengo kuu la Kitengo cha Mipango Miji ni uongozaji wa ukuaji Mji katika misingi endelevu ya kimaendeleo na kimkakati wa ufanisi kiuchumi na kijamii. Shughuli Kuu zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

### 10.2.1 Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mji wa Ushirombo na Runzewe pamoja na Mpango wa uendelezaji Mji kati.

Wataalamu wamekuwa wanaendelea na zoezi la upangaji wa Mji na Mitaa kwa maeneo mbalimbali ya Ushirombo na Runzewe ikiwa ni mkakati wa kuendeleza Mji. Maeneo hayo ni Lyobahika, Ibamba, Kabuhima, Buganzu na Busonzo.

Aidha tumendelea kutoa elimu ya Mipango Mji kwa mwananchi anayefika ofisi ya Mipango Mji kwa ajili ya kupata elimu ya, masuala ya upangaji miji**.** **(Issuance of Development condition)**

Kitengo kimetoa ushauri katika masuala ya uendelezaji wa Mji kadiri wateja walivyojitokeza. Jumla ya wateja (wananchi) 1,500 wamepokea ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia Sheria ya MipangoMiji Na. 8 ya 2007 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 pamoja na Sheria zingine shirikishi.

Kitengo kimetoa masharti ya uendelezaji ambapo jumla ya viwanja 14 vimeadaliwa masharti mbalimbali ya uendelezaji wake kwa kuzingatia sheria na taratibu za uendelezaji **(Development control)**

Pia kitengo kimeshughulikia migogoro 24 ya Ardhi maeneo ya Mjini na Vijijini Bukombe na kuimaliza. Aidha kitengo kinaendelea kushughulikia migogoro kadiri inavyojitokeza.

## 10.3 KITENGO CHA ARDHI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika kipindi hiki cha kuanzia Julai hadi Novemba 2020, Kitengo cha Ardhi kiliendelea na utekelezaji wa kazi za utoaji wa huduma endelevu za ardhi. Shughuli zilizofayika ni kama ifuatavyo:-

### 10.3.1 Uandaaji wa Hati Miliki

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba, jumla ya Rasimu za Hati hamsini 50 ziliandaliwa na kukabidhiwa kwa wamiliki ili zikasainiwe mbele ya Mwanasheria na baadaye kupelekwa kwa Kamishna wa Ardhi ,Mkoani kwa

ajili ya kusainiwa na kusajiliwa. Ambapo kitengo kinatarajia kuandaa hati miliki 3,000 kwa viwanja vyote vilivyopimwa na vinavyoendelea kupimwa Kata ya Katente, Ushirombo, Igulwa, Bukombe, Bulangwa na Uyovu na maeneo mengine ya Bukombe.

**10.4 Makusanyo ya kodi ya Pango la Ardhi**

Kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2020 jumla ya Tzs. 15,051,676.00 sawa na asilimia 5 ya lengo la kukusanya millioni 300,000,000.00 zimekusanywa na kuingizwa kwenye akaunti ya Wizara ya Ardhi.

**10.5 KITENGO CHA UPIMAJI NA RAMANI**

***Mhe. Mwenyekiti;***

Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2020 kitengo cha Upimaji na Ramani kiliendelea na utekelezaji wa kazi zake kama ifuatavyo:

**10.5.1 Upimaji wa Viwanja Vipya**

- Viwanja 1,392 vimepimwa maeneo ya Bukombe katika eneo la Kitangili na Mchangani

**10.5.2 Uchoraji wa Ramani mbalimbali za viwanja**

- Jumla ya ramani 08 za upimaji zimechorwa (survey plans) na zinasubiri uizinishaji wa ramani hizo ili zipitishwe na kusainiwa huko kanda.

## 10.6 KITENGO CHA MISITU

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020 Kitengo cha Misitu kimefanya shughuli zifuatazo;

JEDWALI NA; 30

| NA | SHUGHULI | HALI YA UTEKELEZAJI | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA TENGWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kufanya doria zipatazo 250 ndani na nje ya misitu ya hifadhi ifikapo Juni, 2021. | Doria zipatazo 38 zimefanyika, Gunia za mkaa 1212 ,mbao 604 zilimekamatwa, Baiskeli 13,gari 2 na tela 3 ambazo zilikuwa zinasafirisha mkaa,mbao na magogo zilikamatwa.Pia shoka 9,majembe5,panga 3,punda 6 na msumeno 1 vilikamatwa pamoja tanuru 6 kuteketezwa. | Ruzuku kutoka serikali kuu/oc | 5,114,720/= | 1,279,720/= | 764,240/= | Usimamizi wa maliasili unaendelea kuboreshwa na kuimarishwa |
| 2 | Kukusanya mapato ya Halmashauri kwa mazao yatokanayo na misitu, lengo ni kukusanya Tsh 350,000,000/= ifikapo Juni, 2021. | Jumla ya Tsh 46,077,733.66/= sawa na 13.17% zimekusanywa katika kipindi cha miezi mitatu (Julai – oktoba 2020). | Mapato ya ndani | 4,055,930.33/= | 3,110,000/= | 3,110,000/= | Gharama za ukusanyaji wa mapato zimelipwa. |

## 10.7 KITENGO CHA WANYAMA PORI

***Mhe. Mwenyekiti;***

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020 Kitengo cha Wanyama pori kimefanya shughuli zifuatazo;

JEDWALI NA; 31

| NA | SHUGHULI | HALI YA UTEKELEZAJI | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA TENGWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kufanya doria 5 za kuzuia wanyama waharibifu wa mazao na binadamu ifikapo juni 2021. | -Ufuatiliaji wa Nyati aliyeonekana kijiji cha kazibizyo ulifanyika.<br>-Ufuatliaji wa samba aliyeonekana kijiji cha Namsega na kula ng,ombe watatu ulifanyika, | mapato ya ndani | 1,300,000/= | 420,000/= | 420,000/= | Shughuli itaendelea kutekelezwa kipindi kijacho |

**CHANGAMOTO**

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020 zifuatazo ni baadhi changamoto tulizokutananazo

i. **Idadi ndogo ya Watumishi Idarani**

Idara ina upungufu wa wataalamu ambapo kukosekana na idadi timilifu ya wataalamu inapelekea baadhi ya majukumu ya idara kutofanyika kwa kasi kubwa kutokana na uchache wa watumishi.

ii. **Ukosefu wa maeneo huru ya kupima viwanja**

Halmashauri haina maeneo huru ya kupima viwanja vya matumizi mbalimbali. Elimu inatolewa ili wananchi kuruhusu maeneo yao kupimwa viwanja kwani kuna changamoto ya ukosefu wa fedha za kulipa fidia stahiki na kwa wakati hivyo inabidi kufanya uhamasishaji na kutoa elimu ya namna ya kupanga na kupima maeneo yote ili kuzuia uendelezaji holela lengo likiwa ni kupanga na kupima maeneo yote .

Nawasilisha.

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI IDARA YAMAENDELEO YA JAMII KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2020 – NOVEMBA, 2020

### 11.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Idara hii kwa sasa ina jumla ya Watumishi 8 (ME 3 na KE 5) ambapo watumishi wote wapo Makao Mkuu ya Halmashauri ya Bukombe. Kutokana na ikama ya idara kuna mapungufu ya watumishi 18 kwa ajili ya Kata 17 na mtumishi 01 wa ziada.

### 11.2 MADAWATI YA IDARA

Idara ina madawati sita kama ifuatavyo:-

- Dawati la Ushirikishwaji Jamii
- Dawati la Maendeleo ya Jinsia
- Dawati la Maendeleo ya Mtoto
- Dawati la Uratibu, Ufuatiliaji na Usajili wa NGOs
- Dawati la Kusimamia Masuala Mtambuka
- Dawati la Uwezeshaji Kiuchumi na Kupunguza Umaskini

#### 11.2.1 Dawati la Ushirikishwaji Jamii

*Mhe. Mwenyekiti;*

Dawati hili lina wajibu wa kuratibu, kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu ushirikishwaji jamii katika utatuzi wa changamoto za maendeleo ikiwemo uibuaji wa mipango na miradi inayozingatia vipaumbele vya jamii na Taifa. Vilevilelinaratibu ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za kijamii na kiuchumi zinazotumika katika maandalizi ya mipango shirikishi.

Dawati hili pia linahakikisha kuwa **Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996** inatafsiriwa kwa vitendo ngazi ya jamii ili kuwa na jamii na taifa linalojitegemea. Katika mwaka huu tumetoa mafunzo kuhusu sera ya maendeleo ya jamii katika kata za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Igulwa na Runzewe Magharibi. Pia dawati hili lina kazi ya kuratibu shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

#### 11.2.2 Dawati la Maendeleo ya Jinsia

*Mhe. Mwenyekiti;*

Dawati hili linahusika na kusimamia, kuratibu na kufuatilia uingizwaji wa masuala ya jinsia katika program, mipango na afua mbali mbali za maendeleo katika ngazi ya Halmashauri. Kimsingi dawati linahakikisha Mikataba na Itifaki za Kimataifa iliyoridhiwa na Nchi na kusainiwa kuhusu Haki za Wanawake na **Sera ya Wanawake na Maendeleo ya Jinsia ya Mwaka 2000** zinatafriwa kwa vitendo katika ngazi ya jamii. Kwa mwaka huu dawati hili

limeweza kufanya uhamasishaji kuhusu upingaji wa ukatili wa kijinsia katika jamii na Kujenga uwezo wa jamii kutoa nafasi ya ushiriki sawa katika nafasi za uongozi na utoaji wa maamuzi katika kata za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Igulwa na Runzewe Magharibi.

### 11.2.3 Dawati la Maendeleo ya Mtoto

*Mhe. Mwenyekiti;*

Dawati hili linahusika na kusimamia, kuratibu utekelezaji wa Haki, utoaji wa Elimu ya malezi katika ngazi ya familia na maendeleo ya ujumla kwa mtoto. Kimsingi dawati hili linatekeleza Afua zinahusu Haki na Maendeleo ya Mtoto kama zilivyoainishwa katika Sera, Sheria na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala ya watoto iliyoridhiwa na kusainiwa na serikali. Aidha dawati linajikita katika kuzuia vitendo vyote vinavyosababisha madhara na mmomonyoko wa maadili kwa mtoto.

Dawati hili linahakikisha **Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2008 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009** vinatafsiriwa kwa vitendo ngazi ya jamii. Kwa mwaka huu dawati hili limeweza kuratibu uanzishwaji na uendeshwaji wa Vikundi 10 vya malezi kwa familia katika ngazi ya jamii vyenye jumla ya walezi 171 ambapo Ke ni 89 na Me ni 82. Pia dawati limeweza kutoa elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya mtoto kwa kata za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Igulwa na Runzewe Magharibi.

### 11.2.4 Dawati la Uratibu, Ufuatiliaji na Usajili wa NGOs

*Mhe. Mwenyekiti;*

Kulingana na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2005, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, nchini wameteuliwa na kutumika kama Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Mkoa, Wilaya/Mji. Hivyo Majukumu ya Dawati la NGOs yameanishwa kwa Mujibu Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Dawati linahakikisha **Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001** inatafsiriwa kwa vitendo na wadau wanaofanya kazi ngazi ya jamii na jamii yenyewe. Kwa mwaka huu dawati hili limeweza kuratibu usajili wa Vikundi vya maendeleo vya Kijamii (CBOs) 42.

Pia dawati limeweza kutoa mafunzo ya uendeshaji na uimarishaji wa Vikundi na Kutoa mafunzo kwa vikundi kuhusu Sheria ya fedha ya 2018 na kanuni zake za mwaka 2019 juu ya usajili wa Vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha (HISA) katika kata za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Igulwa na Runzewe Magharibi ambapo jumla ya watu 399 ambapo Ke ni 280 na Me ni 119 wameweza kufikiwa.

### 11.2.5 Dawati la Kusimamia Masuala Mtambuka

*Mhe. Mwenyekiti;*

Masuala mtambuka ni mikakati ya kitaifa inayogusa jamii na kupaswa kutekelezwa na kila sekta na kuitolea taarifa ya utekelezaji. Mikakati hiyo ni pamoja na ule wa UKIMWI, Lishe, Mazingira, Afya. Masuala mtambuka yanakayoratibiwa na dawati hili ni pamoja na UKIMWI, Usajili wa Vizazi na Vifo ngazi ya jamii, lishe, Mazingira na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (CHF).

Katika mwaka huu tumepitia kata zote, vijiji vyote na mitaa yote katika kuwakumbusha majukumu yao kuhusu kamati za kudhibiti UKIMWI. Vile vile shirika la NACOPHA lilitoa mafunzo kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kupitia mradi wao wa HEBU TUYAJENGE. Lengo la mradi huo ni kupunguza maambukizi kwa kufuata taratibu za 95%, 95% na 95%. Aidha, NACOPHA walipita kukagua maendeleo ya miradi ya WAVIU ambapo wamefanikiwa kukagua kikundi cha TUTASHINDA kilichopo kijiji cha Zogolo kata ya BUKOMBE.

Pia tumeweza kusambaza fomu 1400 za usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano (5) kwenye vituo 4 vya kata ya Uyovu, katente, Bulangwa na Bugelenga, Pia fomu 1200 zilikusanywa kutoka kwenye kata hizo.

### 11.2.6 Dawati la Uwezeshaji Kiuchumi na Kupunguza Umaskini

*Mhe. Mwenyekiti;*

Dhumuni kubwa la dawati hili ni kumuwezesha mwananchi kiuchumi ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yanaweza kuwa ni fursa za elimu ya ujasiriamali, fursa za kupata masoko, fursa za maonyesho, fursa za mikopo, fursa za kupata ruzuku kutoka mifuko mbalimbali inayotambulika na Baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Katika mwaka huu, tulitoa mikopo ya Tsh 73,100,000 kwa Vikundi 24 vya wajasiriamali Wanawake na Vijana. Vile vile tulizungukia Kata sita za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Runzewe Magharibi na Igulwa kuhamasisha uundaji wa Vikundi vya Ujasiriamali ili viweze kusajiliwa na kuchangamkia fursa mbali mbali ambapo jumla ya watu 399 ambapo Ke ni 280 na Me ni 119 wameweza kufikiwa.

## 11.3 TAARIFA YA UTOAJI MIKOPO

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba Kiasi cha Tshs. 73,100,000.00 kimekopeshwa katika Vikundi 24 vya wajasiriamali Wanawake (20) na Vijana

(04) kwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii. Mchanganuo wa Vikundi hivyo nikama Ifuatavyo;

**I. JEDWALI NA; 32 - KUPITIA MAPATO YA NDANI**

| Na | JINA LA KIKUNDI | KATA | SHUGHULI | AINA YA KIKUNDI | KIASI KOPESHWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Maendeleo | Igulwa | Ununuzi & uuzaji wa mazao | Kikundi cha Vijana | 1,000,000 |
| 2 | Umoja na Mshikamano | Bukombe | Hisa | Kikundi cha Vijana | 5,000,000 |
| 3 | Tujikwamue | Katente | Ufugaji wa Kuku na Uchimbaji wa Madini | Kikundi cha Vijana | 8,000,000 |
| 4 | Akina mama Tunaweza | Igulwa | Hisa/ Upondaji wa kokoto na ufugaji wa kuku | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 5 | Faraja | Bulangwa | Ufugaji na Biashara | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 6 | Muungano | Katente | Ufugaji kuku & Nguruwe | Kikundi cha Wanawake | 1,100,000 |
| 7 | Furaha | Bukombe | Kilimo na biashara ndogo ndogo | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 8 | Umoja wa kilimo | Bulangwa | Hisa, Kilimo & Ufugaji | Kikundi cha Wanawake | 4,000,000 |
| 9 | Courtesy | Katente | Ufugaji & Ununuzi wa Nafaka | Kikundi cha Wanawake | 9,000,000 |
| 10 | Wamama wa Nguvu | Igulwa | Ufugaji kuku & Nguruwe | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| **JUMLA** | | | | | **36,100,000** |

**II. JEDWALI NA; 33 - KUPITIA FEDHA ZA MZUNGUKO (REVOLVING FUND)**

| Na | JINA LA KIKUNDI | KATA | SHUGHULI | AINA YA KIKUNDI | KIASI KOPESHWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fadhila | Igulwa | Hisa/ Ujasiliamali | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 2 | Upendo | Bulangwa | Ufugaji wa Nguruwe | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 3 | Upendo businda | Ushirombo | Kilimo cha mpunga & Businda | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 4 | Ushirikiano Group | Igulwa | Hisa/ Biashara ndogo ndogo | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 5 | Amani | Busonzo | Hisa na Ufugaji wa Mbuzi | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 6 | Juhudi | Namonge | Hisa na Ufugaji wa Mbuzi | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 7 | Nyota Njema | R: Magaharibi | Hisa | Kikundi cha Wanawake | 3,000,000 |
| 8 | Nyikonga | R: Mashariki | Ununuzi & Uuzaji wa Asali | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 9 | Wamama Wa Nguvu | Igulwa | Biashara ya nafaka, Bustani | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 10 | Tuinuane | R: Mashariki | Hisa/ Biashara ya nafaka | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 11 | Wajasiliamali Wakulima | Igulwa | Hisa/ Uuzaji wa mchele | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 12 | Mshikamano | R: Mashariki | Ushonaji | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| 13 | Wajane | Uyovu | Kilimo | Kikundi cha Wanawake | 2,000,000 |
| **JUMLA** | | | | | **27,000,000** |

**III. JEDWALI NA; 34 - KUPITIA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI**

| Na | JINA LA KIKUNDI | KATA | SHUGHULI | AINA YA KIKUNDI | KIASI KOPESHWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bora Kilimo Biashara | Uyovu | Uchakataji wa mazao | Kikundi cha Vijana | 10,000,000 |
| **JUMLA** | | | | | **10,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | | | | **73,100,000** |

Vikundi hivyo 04 vya Vijana vimekopeshwa jumla ya **Tsh 24,000,000** na Vikundi 20 vya Wanawake vimekopeshwa Jumla ya **Tsh 49,100,000**.

Aidha katika kipindi cha mwaka huu, Halmashauri imefanya ufuatiliaji wa marejesho ya Vikundi vinavyodaiwa na kukusanya jumla **Tsh 13,726,500.** Vile vile, tumesajili jumla ya Vikundi 42 vya wajasiriamali vya Wanawake, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Vikundi Mchanganyiko.

### 11.4 TASAF III

***Mhe. Mwenyekiti;***

Mpango wa TASAF III ambao unatekelezwa Wilayani Bukombe unahudumia kaya 5,058 katika vijiji 42 hapa Wilayani. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020 Halmashauri ya Wilaya ilipokea kiasi cha Tshs. 236,454,360.00 kwa ajili ya Malipo kwa Kaya Maskini (Tshs. 220,096,000.00) na Usimamizi na Ufuatiliaji wa zoezi hili (Tshs. 16,358,360.00)

Matumizi ya Fedha hizo nika ifuatavyo;

a) Malipo ya walengwa **2,965** yalifanyika kwa kiasi cha **Tshs. 219,984,640.00**
b) Usimamizi na Ufuatiliaji Ngazi ya Wilaya na Kata kiasi cha **Tshs. 16,358,360.00**

Pia zoezi la uhakiki wa Walengwa wa Mpango wa TASAF III ulifanyika Julai,2020 na utafanyika tena tarehe 30 Disemba, 2020. Lengo ni Kuondoa Walengwa wasio na Sifa (Walikufa, Walihama, Kaya zao sio Maskini sana)

### 11.5 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI NYINGINE

***Mhe. Mwenyekiti;***

Zifutazo ni baadhi ya shughuli nyingine zilizofanywa na Idara ya Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020:-

- Usajili wa vikundi vya ujasiriamali
- Ufuatiliaji wa Marejesho ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.
- Kuamsha ari kwa Wananchi kushiriki kwenye Uchumi wa Viwanda
- Kutoa elimu ya mapambano dhidi ya UKIMWI pamoja na kukumbusha majukumu ya kamati za kudhibiti UKIMWI kwa kila Kata, Mitaa na Vijiji.
- Kutoa elimu ya uundaji wa Vikundi kwa wananchi wa kila Kata, Vijji na Mitaa.
- Kufanya uhakiki wa vikundi vilivyoomba mkopo kupitia mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

- Kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.
- Kutoa mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu
- Kutoa mafunzo kwa vikundi kuhusu Sheria ya fedha ya 2018 na kanuni zake za mwaka 2019 juu ya usajili wa Vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha (HISA) katika kata za Namonge, Uyovu, Busonzo, Runzewe Mashariki, Igulwa na Runzewe Magharibi.

## 11.4 CHANGAMOTO

***Mhe. Mwenyekiti;***

Idara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:-

- Kata zote 17 hazina wataalamu wa kada ya maendeleo ya jamii
- Mahitaji ya mikopo ni mengi sana ukilinganisha na fedha inayotengwa.
- Vikundi vilivyokopeshwa fedha baadhi yao kutorejesha kwa wakati hasa vikundi vya Vijana na watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa bajeti ya kufanya ufuatiliaji (Monitoring and evaluation) kwa Vikundi vilivyokopeshwa ili kuweza kujua maendeleo na changamoto zinazowakabili katika ufanyaji kazi wao kwenye miradi yao hasa waliyoombea mikopo kutoka halmashauri
- Idara haina usafiri wa uhakika kuweza kuendesha shughuli za Idara.
- Vikundi vilivyokopa havifanyi marejesho kulingana na Mikataba yao hivyo kushindwa kutoa fedha kwa vikundi vingine kwani fedha nyingi zinakuwa kwa vikundi visivyorejesha.

## 11.5 MIKAKATI

- Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana, watu wenye Ulemavu na wanawake kwa kufuata sheria zilizopo
- Kufanya ufuatiliaji wa marejesho kwa wanaochelewesha kurejesha kwa wakati kulingana na upatikanaji wa bajeti ya ufuatiliaji
- Kuomba kibali cha kuajiri watumishi wengine wa kada ya maendeleo ya jamii.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA IDARA YA UJENZI KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI, 2020 – NOVEMBA, 2020**

## 12.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Idara ya Ujenzi ni Idara mtambuka inatoa huduma usimamizi wa ujenzi na matengenezo ya miundombinu na mitambo katika Sekta mbalimbali katika Halmashauri kupitia vitengo viwili vilivyo katika Idara.

i. Kitengo cha Majengo
ii. Kitengo cha Mitambo

## 12.1 WATUMISHI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Idara inatakiwa kuwa na jumla ya Wataalamu 11 kwa sasa ina Watumishi 6 na hivyo kuwa na upungufu wa Watumishi 5

***Jedwali 35 -: Hali ya Watumishi***

| **Na.** | **Fani** | **Mahitaji** | **Watumishi waliopo** | **Mapungufu** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wahandisi | 2 | 1 | 1 |
| 2 | Msanifu Majengo | 2 | 0 | 2 |
| 3 | Mkadiriaji Majengo | 2 | 0 | 2 |
| 4 | Fundi sanifu | 4 | 4 | 0 |
| 5 | Mhudumu | 1 | 1 | 0 |
| | **Jumla** | 11 | 6 | 5 |

## 12.2 KAZI TEKELEZWA JULAI HADI NOVEMBA 2020

*Mhe. Mwenyekiti*

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020, Idara ililenga;

i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma kwa kusimamia ujenzi wa majengo ya Serikali, Taasisi na watu binafsi ili kuhakikisha majengo yote yanajengwa kwa ubora unaokubalika.
ii. Idara iliendelea na kazi ya kukagua na kufanya matengenezo magari ya Serikali ili kukidhi mahitaji ya usafiri na usafirishaji katika Halmashauri.

## 12.3 CHANGAMOTO

*Mhe. Mwenyekiti*

Idara imekumbana na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa kazi tajwa hapo juu:

**1.** Upungufu wa vitendea kazi kama vile usafiri ili kuwawezesha wataalam kufanya ukaguzi na usimamizi wa miradi kwa karibu.

2. Upungufu wa wataalamu katika Idara ya Ujenzi wa Kusanifu, Kukadiria na kusimamia miradi na Kitengo cha Mitambo kukosa kabisa wataalamu kwa fani za Umeme, Maji na Mitambo.
3. Ukosefu wa fedha za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi inayotekelezwa.

**12.6 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

i. Kuomba kibali cha ajira kwa kada zinazohitajika.
ii. Kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa.
iii. Kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi.

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020**

## 13.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti*

Kitengo cha Sheria, ni miongoni mwa vitengo 06 zilizo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Kiutawala.

## 13.1 Hali ya Utumishi

*Mhe. Mwenyekiti*

Kitengo hiki kina jumla ya Watumishi (Wataalam) Wawili (2) ambao wote ni wanasheria hivyo kitengo kina Upungufu wa wanasheria wawili.

### 13.1.1 Majukumu ya Kitengo

Majukumu makuu ya Kitengo hiki ni kama ifuatavyo:-

- Kutoa ushauri wa kisheria kwa Halmashauri na kuiwakilisha Halmashauri katika mashauri mbalimbali Mahakamani.
- Kuandaa mikataba na kuishauri Halmashauri katika masuala ya mikataba na kuandaa Sheria Ndogo za Halmashauri.
- Kupitisha na kuwasilisha kwa Mkurugenzi mapendekezo ya Sheria ndogo za Vijiji.
- Kushauri idara nyingine zote zilizopo katika Halmashauri juu ya masuala yote yanayohusu sheria.
- Kuelimisha Umma kuhusu Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria kwa ujumla.
- Kuratibu uendeshaji wa Mabaraza ya Kata, kutayarisha na kuandaa semina zinazohusu masuala ya kisheria.
- Kusimamia uandishi wa nyaraka mbalimbali za kisheria.
- Kutunza kumbukumbu za mashauri yaliyopo Mahakamani.
- Kushiriki katika majadiliano na Mikutano mbalimbali ambayo inahitaji utaalamu wa kisheria.
- Kutoa msaada wa kisheria kwa jamii yote iliyopo ndani ya Halmashauri.
- Kutoa elimu kwa Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata kuhusu Utawala Bora katika kutoa maamuzi hasa kuzingatia haki ya kusikilizwa, kutokuwa na upendeleo na kuzingatia usawa katika utoaji wa huduma kwa wananchi.
- Kuanzisha na kufanya mabadiliko ya Sheria Ndogo za Halmashauri za ukusanyaji wa ada na ushuru na kutoa mapendekezo ya mabadiliko kupitia ngazi ya Halmashauri, Mkoa na Wizara.
- Kufanya upekuzi wa mikataba na kufanya marekebisho kabla ya kusainiwa kwa utekelezaji kwa ajili ya utoaji huduma kwa wananchi iliyoletwa na Watendaji wa Vijiji, Kata na Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Wasimamizi wa Zahanati.

- Kutoa ushauri kwa Halmashauri kwa mashauri ya nidhamu za watumishi ikiwa ni pamoja na kusimamia Sheria za Utumishi wa Umma kwa uadilifu.
- Kutatua migogoro ya ardhi kwa kutoa ushauri baina ya mtu na Kijiji au Kijiji na Kijiji.
- Kuhakikisha Sheria ya Fedha na Mapato ya Serikali za Mitaa zinatekelezwa kwa uadilifu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ya tabia ya kulipa tozo mbalimbali kwa Serikali.

**13.2 Utendaji kazi Julai – Novemba, 2020**

***Mhe. Mwenyekiti***

Miongoni mwa kazi zilizofanywa na Kitengo hiki katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka ni:-

- Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Halmashauri.
- Kuratibu na kuyasimamia Mabaraza ya Kata yote 17 ya Halmashauri ya BUKOMBE.
- Kuandaa Mikataba mizuri na iliyotengenezwa kwa wakati kwa asilimia mia moja.
- Kujenga uwezo kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata ambapo mabaraza 8 kati 17 yalifikiwa.
- Kutoa hati za madai kwa mujibu wa Sheria zinazohusu madeni ya tozo mbalimbali.
- Kuiwakilisha Halmashauri Mahakamani kwa uadilifu mkubwa.
- Kusimamia Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria Mama kwa uaminifu mkubwa katika maeneo yote.

**13.3 TAARIFA ZA KESI**

***Mhe. Mwenyekiti***

- Kuanzia Julai 01, 2020 hadi kufikia Novemba 24, 2020 Halmashauri ilikuwa na kesi nne (04) ambazo zipo kwenye hatua za kutajwa na kusikilizwa kwenye Mahakama mbalimbali. (Jedwali limeambatanishwa la mchanganuo wa kesi)

**13.4 CHANGAMOTO**

- Mabaraza ya Kata kutokuwa huru kiutendaji.
- Ukiukwaji wa Sheria kwa makusudi kwa Wananchi.

**13.4.1 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO**

- Kupunguza idadi ya Kesi kwa 80% hadi 2020/2021 dhidi ya Halmashauri kwa kutumia njia ya mazungumzo (Alternative Dispute Resolution).
- Kuendelea kuwajengea uwezo viongozi wa Vijiji na Halmashauri kupitia vikao mbalimbali.
- Kuendelea kuchukua hatua kwa wakati pindi linapotokea jambo.

- Kujiridhisha mara kwa mara na Sheria mpya au maboresho ya Sheria.
- Kuhakikisha wajumbe wote waliopata mafunzo wanajengewa uwezo wa kuendesha Mabaraza ya Kata.
- Kuendelea kuboresha Miongozo na Sheria zinazoongoza utoaji haki katika Mabaraza kwa lugha rahisi.
- Halmashauri wa Bukombe kupitia Kitengo cha Sheria inaamini katika misingi ya Utawala Bora kama nyenzo muhimu ya kusukuma maendeleo ya wananchi mbele. Utawala Bora unaweza kusaidia sana katika kupunguza umaskini kutokana na wananchi wote kushiriki katika mchakato wa upangaji mipango ya uchumi wao na rasilimali kutumiwa vizuri
- Ili kujenga Utawala Bora Halmashauri itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya utii wa sheria haki na wajibu wao kama raia na kuwashauri na kuwahamasisha kushiriki katika shughuli za maendeleo na hata shughuli binafsi za uzalishaji mali na vilevile umuhimu wa kulipa tozo mbalimbali kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Halmashauri hasa zile zinazohusu Usafi wa Mazingira na za Ada na Ushuru.
- Kuendelea kuwaelimisha Wananchi na kuwapa ufafanuzi kuhusu Sheria Ndogo za Halmashauri

**JEDWALI NA; 36 - MCHANGANUO WA MASHAURI YALIYOPO MAHAKAMANI/BARAZA/MAHAKAMA YA USULUHISHI KWA HALMASHAURI YA BUKOMBE KUANZIA JULAI, 01 2020 HADI NOVEMBA 2020.**

| NA | SHAURI NA MAHAKAMA LILIPO | CHANZO CHA MADAI | KIASI KINACHODAIWA | HATUA ILIYO FIKIWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Clement Misungwi na Wenzake 3 dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe Na. 21/2015. Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Shinyanga | Madai ya fidia baada ya ardhi yao kutwaliwa na serikali ya kijiji cha Bulugala kwa ajili ya kujenga shule ya Sekondari Nyasato katika kata ya Nyasato | Tshs 21,893,024/= kama fidia | Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe imeamriwa kuwalipa wadai fedha iliyodaiwa/fidia ya usumbufu pamoja na gharama za kesi hiyo. | Shauri bado linaendelea kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Shinyanga |
| 2. | Thabita Petro Mwasi dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Na. 124/2016, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kahama | Madai ya fidia ya Ardhi ambapo mdai anadai kuwa Halmashauri ilipitisha barabara kwenye eneo lake bila kumlipa fidia. | Tshs. 45,000,000/= | Shauri hili limekwisha | Halmashauri imeshinda |

| NA | SHAURI NA MAHAKAMA LILIPO | CHANZO CHA MADAI | KIASI KINACHODAIWA | HATUA ILIYO FIKIWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Robert Rafael Katabanya dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Na. 119/2017, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kahama | Madai ya ardhi ambayo alipewa na Serikali ya kijiji cha Igulwa mwaka 1982 ambapo mdai anadai kuwa Halmashauri ilichukua eneo lake na kujenga ofisi za makao makuu ya Halmashauri na nyumba za watumishi/ Sehemu ya eneo la hospitali ya Wilaya bila kumlipa fidia | Thamani ya eneo ni 30,000,000/= lakini mdai anadai Halmashauri imrudishie eneo lake na siyo fidia. | Shauri limekwisha | Halmashauri imeshinda |
| 4. | Kambarage Garage dhidi ya DED- Bukombe | Madai ya matengenezo ya Magari | Kambarage Garage anaidai Halmashauri Milioni tisini | Kesi inaendelea katika hatua za usuluhishi | Shauri bado linaendelea |

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha.

**TAARIFA YA KITENGO CHA TEHAMA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020**

## 14.0 MUUNDO WA KITENGO CHA TEHAMA

*Mhe. Mwenyekiti*

Kitengo cha TEHAMA ni kitengo kati ya vitengo sita vyenye hadhi ya idara katika halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kinachotoa huduma ya ya usimamizi wa mifumo ya TEHAMA na kuhabarisha wananchi juu ya mambo yote yanayofanywa na serikali. Kitengo cha TEHAMA kina jumla ya watumishi 3 ambapo Mtumishi 01 ni Afisa Habari na watumishi 02 ni Maafisa TEHAMA.

## 14.1 MAJUKUMU YA KITENGO

i. Kusimamia mifumo yote ya TEHAMA na njia zote za Mawasiliano katika Halmashauri.

ii. Kusimamia na kuhakikisha kuwa vyombo vyote vinavyohusiana na TEHAMA vinafanya kazi na vinakuwa katika hali nzuri.

iii. Kufanya utafiti kwenye mifumo mbalimbali ya Komputa ndani na nje ya Halmashauri kisha kutoa ushauri na mapendekezo na kuiwasilisha kwenye kikao cha menejimenti (CMT) na kamati za kudumu kwa ajili ya utekelezaji.

iv. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya taratibu za utendaji kazi za kila siku za halmashauri, kisha kubaini matatizo yaliyomo na kubuni mifumo mbalimbali ya komputa itakayowezesha kutatua matatizo hayo.

v. Kuiongoza halmashauri kwenye mipango yote ya baadae inayohusiana na TEHAMA na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na msaada wa kutosha kwa watumiaji wa komputa kuhusiana na mifumo mbalimbali (LGRCIS, EPICOR, GoTHOMIS, LAWSON na FFARS.

vi. Kutayarisha na kutunza miongozo na sera za halmashauri za TEHAMA na kusimamia sera ya Taifa ya TEHAMA.

vii. Kukusanya na kuandika Habari.

## 14.2 KAZI ZILIZOFANYIKA KATIKA KIPINDI CHA JULAI HADI NOVEMBA 2020.

*Mhe. Mwenyekiti*

1. **Utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA**

Kitengo kimetengeneza mashine nukushi (fax) katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, computer 10 printer 04 Scanner 02 katika idara mbalimbali na bado kitengo kinaendelea kufanya matengenezo madogo madogo kulingana na miongozo mbalimbali ya serikali na Halmashauri.

2. **Ufungaji wa mtandao kiambo (LAN)**
   Kitengo kimefunga mtandao kiambo (LAN) kwenye Kituo cha Afya Uyovu, Kituo cha Afya Ushirombo na hospitali ya Wilaya ya Bukombe kwa ajili ya ufungaji wa mfumo wa GoTHOMIS.

3. **Kusimika na kuratibu mfumo wa GoTHOMIS katika vituo vya kutolea huduma za Afya**
   Mfumo wa utoaji taarifa na ukusanyaji wa mapato (GoTHOMIS) umefungwa na kutolewa mafunzo kwa watumiaji katika Zahanati ya Iyogelo, kituo cha Afya Ushirombo na Hospitali ya Wilaya ya Bukombe.

4. **Kusimamia na kuratibu usajili wa watumiaji wa mfumo wa vitambulisho vya ujasiriamali**
   Tumeweza kusajili watumiaji wa mfumo wa vitambulisho vya ujasiliamali ambapo mpaka sasa jumla ya watumiaji 6113 wameshasajiliwa na vilevile tumeweza kuwapa mafunzo timu ya uuzaji vitambulisho kwa ajili ya kusajili wajasiliamali wadogowadogo (Machinga)

5. **Kusimamia vifaa vya ukusanyaji mapato (POS)**
   Kwa kushirikiana na idara ya fedha Kitengo kimeendelea kusimamia vifaa vya ukusanyaji mapato (POS), kusajili watumiaji wapya wa ukusanyaji wa mapato, kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa mapato kwa watumiaji na kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za vifaa hivyo ili kuweza kukusanya mapato kwa wakati.

6. **Kusimamia Tovuti ya Halmashauri Pamoja na mitandao mingine ya kijamii**
   Kitengo kimeendelea kusimamia, kuboresha na kuhuisha habari zinaandikwa na kuwekwa katika Tovuti ya halmashauri inayopatikana kwa kiunganishi cha www.bukombedc.go.tz pamoja na mitandao mingine ya kijamii kama **Facebook**: Bukombe District Council, **Twitter:** Bukombe District Council, **Instagram:** Bukombe District Council kwa mujibu wa taratibu na maelelekezo ya Serikali.

7. **Kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Madenimis**
   Kwa kushirikiana na idara za Utumishi, Elimu Sekondari na Msingi, Kitengo kimetoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa **Madenimis** kwa walimu wote wa Shule za Msingi na Sekondari katika Halmashauri ya BUKOMBE. Tayari walimu wote wana uwezo wa kutumia mfumo huo kwa ajili ya kuomba madai yao yasiyokuwa ya mshahara kupitia mfumo huo, vile vile tumeweza kusajili walimu wapatao 122.

8. **Kupiga picha na kutengeneza vitambulisho vya Bima ya Afya kwa Wazee.** Kwa kushirikiana na Idara ya Afya, Kitengo kimefanikiwa kupiga picha na kutengeneza vitambulisho vya Bima ya Afya kwa wazee 930.

9. **Kusimamia ujumlishaji wa kura wakati wa Uchaguzi** Kwa kushirikiana na Wasimamizi wa uchaguzi, Kitengo kilipokea mafunzo ya mfumo wa **Result Management System** wa NEC kwa ajili ya kujumlisha matokea ya kura wakati wa Uchaguzi, kazi ambayo ilifanyika kwa ufanisi na kwa wakati.

10. **Ufungaji wa kamera katika duka la dawa hospitali ya wilaya ya Bukombe.** Kwa kushirikiana na Idara ya afya, kitengo kimeweza kufunga kamera katika duka la dawa katika hospitali ya Wilaya ya Bukombe kwa ajili ya kudhibiti wizi wa dawa.

## 14.3 MAFANIKIO

*Mhe. Mwenyekiti*

i. Kuwezesha kutoa taarifa sahihi na za haraka za kifedha za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa mapato (LGRCIS), GoTHOMIS na mfumo wa matumizi wa EPICOR.
ii. Kutoa risiti na nyaraka mbalimbali za kifedha zinapohitajika kwa haraka
iii. Kudhibiti au kupunguza makosa yaliyojitokeza katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vitabu
iv. Makusanyo kuongezeka kutokana na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika Vituoni vya afya na Hospitali ya Wilaya kutokana na matumizi ya mfumo wa GoTHOMIS baada ya kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mfumo.)
v. Kupungua kwa changamoto za upotevu wa taarifa miongoni mwa watumiaji wa Computer.
vi. Watumishi kutumia mfumo wa madenimis kwa ajili ya kuweka kumbukumbu zao za madeni kwenda wizara ya utumishi na utawala bora.
vii. Kuwa na takwimu sahihi za wajasiriamali wadogowadogo ambao wanatambulika Tanzania nzima.
viii. Kwa matumizi ya mfumo wa Result Management System (RMS) Matokeo kwenye uchaguzi wa madiwani, wabunge na Rais yalitoka kwa wakati na kupunguza malalamiko toka kwa vyama vya Siasa.

### 14.4 CHANGAMOTO

i. Uelewa mdogo wa matumizi ya TEHAMA kwa watumiaji wa Mfumo.
ii. Kukatikakatka kwa huduma ya mawasiliano ya mtandao kutokana na kutumia teknolojia ya Dish (VSAT).

### 14.5 MIKAKATI

i. Kutoa elimu na kugawa miongozo mbalimbali ya matumizi bora na salama ya TEHAMA.
ii. Kuendelea kuwasiliana na TAMISEMI kwa ajili ya upatikanaji wa mtandao kwa wakati.
iii. Kuendelea kuimarisha mtandao wa ndani LAN ili kuwezesha upatikanaji wa mifumo kwa wakati.
iv. Kuunganisha mifumo kwenye Mkonga wa Taifa.
v. Kuunganisha mfumo wa makusanyo (GoTHOMIS) Kwenye zahanati za Iyogelo, Bugando, Miyenze, Businda na Ikuzi.

***Mhe. Mwenyekiti***

Nawasilisha

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KITENGO CHA MANUNUZI KWA KIPINDI KUANZIA MWEZI JULAI HADI Novemba 2020**

## 15.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Kitengo cha Manunuzi, ni miongoni mwa Vitengo 06 zilizo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Kiutawala.

## 15.1 Hali ya Utumishi

Kitengo hiki kina jumla ya Watumishi (Wataalam) 09 ambao ambapo mmoja ni Afisa Manunuzi 04 na 05 ni Maafisa manunuzi wasaidizi.

## 15.2 MAJUKUMU MAKUU YA KITENGO CHA MANUNUZI.

1. Kusimamia manunuzi ya Halmashauri
2. Kusimamia shughuli zote za Ugavi
3. Kutunza kumbukumbu za Ununuzi na Ugavi
4. Kuandaa nyaraka za zabuni na mikataba ya Ununuzi
5. Kuandaa Mpango wa manunuzi wa Halmashauri

## 15.3 UTENDAJI KAZI WA KITENGO CHA MANUNUZI KIPINDI CHA JULAI - NOVEMBA 2020

*Mhe. Mwenyekiti;*

Miongoni mwa kazi zilizofanywa na Kitengo hiki katika kipindi cha Julai 2020 - Novemba, 2020 ni:-

1. Kuandaa mpango wa manunuzi wa Halmashauri
2. kusimamia kazi ya ununuzi wa vifaa ambavyo vimo katika makisio na mpango wa ununuzi
3. kusimamia upatikanaji wa vifaa kutoka kwa wazabuni mbalimbali
4. kutunza ghala na kumbukumbu za vifaa
5. kupokea vifaa vipya vitakavyoletwa na wazabuni
6. kupokea vifaa vilivyotumika lakini vinahitaji kutunzwa kabla ya kufutwa.
7. Kuandaa nyaraka za zabuni mbalimbali na mikataba
8. Kushauri na kusimamia ngazi za msingi katika masuala ya manunuzi.
9. Kupokea na Kutunza vifaa kutoka tume ya Taifa ya Uchaguzi.
10. Kupanga na kusambaza vifaa kwa ajili ya zoezi la Uchaguzi Mkuu
11. Kutunza vifaa vilivyobaki baada ya Zoezi la Uchaguzi Mkuu

*Mhe. Mwenyekiti;*

Nawasilisha.

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020**

## 16.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Kwa mujibu wa kifungu Na. 48 cha Local Government Financies act No. 9/1982 kikisomwa pamoja na kifungu cha 14(4) cha Local Authority Financial Memorandum ya mwaka 2009. Ni wajibu wa Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri kuangalia, kupima na kutoa taarifa juu ya udhibiti wa ndani kama unatekelezwa vizuri na kwamba mali za Halmashauri zinatumika vizuri bila hasara kwa Halmashauri na ufanisi unaotakiwa, pamoja na mwongozo wa ukaguzi wa ndani "Local Government internal Audit manual ya mwaka 2013 na miongozo mingine iliyotolewa na Bodi ya wahasibu na wakaguzi Tanzania (NBAA).

## 16.1 Muundo wa Ukaguzi

*Mhe. Mwenyekiti;*

Ukaguzi wa Akaunti zote za Halmashauri umefanyika kwa kuangalia mapato na matumizi, manunuzi, na miradi ya maendeleo kwa kupitia nyaraka mbalimbali ikiwemo mapato yaliyokusanywa kwenye mfumo wa mapato (LGRCS), matumizi kwa kupitia hati za Malipo na viambatanisho vyake na miradi mbalimbali iliyotekelezwa kuanzia mwezi 01.07.2020 hadi tarehe 25.11.2020 pia tulipitia nyaraka za manunuzi kama vitabu vya stoo, pamoja na mfumo ya udhibiti wa ndani wa halmashauri kwa ujumla.

### 16.1.1 Malengo ya Ukaguzi

- Kumuwezesha mkaguzi wa Ndani kutoa maoni yake juu ya udhibiti wa Mfumo wa ndani (Internal control system)
- Kuangalia na kuthibitisha kama Fedha zote zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa tu na si vinginevyo (Approved budget).
- Kuthibitisha kama bidhaa na huduma zilizonunuliwa zinapatikana kwa kutumia sheria za manunuzi Na 21 ya mwaka 2011.
- Kuangalia Kama nyaraka zote za malipo zimeidhinishwa kwa utaratibu unaokubalika na zinatunzwa baada ya malipo.
- Kuangalia Kama taratibu, sheria na kanuni zote za matumizi ya fedha za Halmashauri zinafuatwa kikamilifu.
- Kuangalia kama Fedha zote zilizokusanywa zinapelekwa Benki kabla ya kuzitumia
- Kuthibitisha kama Ushuluhisho wa kibenki unafanyika kwa wakati unaotakiwa, ndani ya siku 15 baada ya mwezi kuisha.
- Kuhakikisha Kama Halmashauri inatekeleza mapendekezo yaliyotolewa na mkaguzi wa ndani katika Robo iliyopita.

- Kuangalia thamani ya fedha kwenye miradi na ubora wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani na serikali kuu.
- Kuangalia kama fedha za mapato ya ndani zinapelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

### 16.1.2 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI (AUDIT METHODOLOGY).

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na kumbukumbu zake, mbinu za ukaguzi wa hesabu na utaratibu zilizotumika ni kama ifuatavyo:

- Kupitia kanuni za Halmashauri, miongozo na nyaraka nyingine za Halmashauri.
- Kuchunguza stakabadhi za malipo ili kuthibitisha ukubalifu sheria zilizopo, kanuni za fedha, maelekezo au maagizo mengine.
- Kufanya majaribio ya ulinganifu katika mfumo wa kutoa mikataba na utekelezaji wake.
- Kufanya ukaguzi wa eneo husika ili kuthibitisha utekelezaji halisi wa shughuli zilizopangwa pamoja na kutathimini mafanikio yaliyo patikana.

### 16.2 Changamoto

- Kitengo kinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati kwa kutokuwa na usafiri maalum wa kitengo.
- Bajeti isiyotosheleza kuendesha shughuli za kitengo cha ukaguzi wa ndani

### 16.2.1 NJIA ZA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO

- Kitengo kinashirikiana vizuri na idara nyingine ili kuweza kupata usafiri kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake pamoja na gharama nyingine za ukaguzi.

### 16.2.2 Mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi

*Mhe. Mwenyekiti;*

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa maeneo mengi yamefanya vizuri kwa kuzingatia taratibu, miongozo, sheria, kanuni na sheria ndogo za Halmashauri isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo yalibainika kuwa na kasoro mbalimbali za kiutendaji ambazo tumezitolea ushauri na mapendekezo yetu.

Hata hivyo jumla ya hoja 89 ziliibuliwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na robo ya kwanza (julai hadi septemba 2020) kati ya hizo hoja zilifanyiwa kazi na kufungwa sawa na asilimia 45.46%na hoja ambazo zilizoko katika utekelezaji ni 54.54%.Pia ufafanuzi kwa kila mwaka na hoja zilizoibuliwa ni kama inavyoonekana katika hapo chini.

**Jedwali Na; 37 – UTEKELEZAJI KWA KILA HOJA**

| KIPINDI | | HOJA | UTEKELEZAJI KWA KILA HOJA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Zimetekelezwa | Inaendelea kutekelezwa | Hazijatekelezwa | Zimefungwa | Hazijafungwa |
| **Mwaka** | **Robo** | **Idadi** | **Idadi** | **Idadi** | **Idadi** | **Idadi** | **Idadi** |
| **2019/2020** | **I - IV** | 89 | 35 | 50 | 4 | 35 | 54 |
| **2020/2021** | **1** | 22 | 15 | 5 | 2 | 15 | 7 |
| **JUMLA KUU** | | **110** | **50** | **55** | **6** | **50** | **61** |

## 16.3 Hitimisho

***Mhe. Mwenyekiti;***

Mambo yaliyobainika kuwa na upungufu au kasoro katika zoezi la ukaguzi yanaweza kuepukika kama wahusika watazingatia taratibu, kanuni na sheria katika utekelezaji wa majukumu yao na Halmashauri kutekeleza yale majukumu yaliyo katika ngazi ya Halmashauri. Mwisho tunapenda kutoa shukrani zetu kwa uongozi wa Halmashauri, na wafanyakazi wote ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia katika kufanikisha taarifa hii ya ukaguzi.

***Mhe. Mwenyekiti;***

Nawasilisha

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KITENGO CHA NYUKI KWA KIPINDI KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020

### 17.0 UTANGULIZI

Wakazi wa Wilaya ya Bukombe kwa asili wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki na hii ni kutokana na kuwa na Manzuki nzuri na yakutosha. Wilaya imezungukwa na misitu ya Asili ambayo ni Msitu wa Ushirombo, Msitu wa Bukombe/Mbongwe, Msitu wa Kahama/Biharamulo pamoja na Hifadhi wa Wanyamapori Kigosi/Myovosi.

Maeneo haya yote yana misitu ya miombo hivyo kufanya kuwa na Manzuki nzuri na yakuvutia kwa nyuki. Kutokana na hali hiyo imeifanya Wilaya Bukombe kuwa moja ya wilaya chache zinazozalisha asali mahuluku na kwa wingi nchini Tanzania.

### 17.1 MAJUKUMU YA KITENGO CHA NYUKI

**Idara hii inajihusisha na majikumu yafuatayo;**

- **i.** Kuhamasisha njia bora za ufugaji nyuki ndani ya Wilaya.
- ii. Kuhamasisha jamii Kuhusu ubora na usalama wa mazao ya nyuki
- iii. Kuimarisha uwezo wa jamii katika kusimamia na matumizi ya sheria, kanuni na sera za ufugaji nyuki.
- iv. Kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki bora wa kisasa kwa vikundi vya ufugaji nyuki, taasisi na watu binafsi.
- v. Kukusanya takwimu sahihi za wafugaji Nyuki pamoja na uzalishaji
- vi. Kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali
- vii. Kutoa Elimu za Ufugaji Nyuki wa Kisasa
- viii. Kusimamia na kuwapa elimu wafanyabiashara na wadau wa mazao ya Nyuki juu ya ubora wa mazao ya Nyuki

### 17.2 TAARIFA YA UJENZI WA KIWANDA CHA KUCHAKATA NA KUFUNGASHA MAZAO YA NYUKI KUFIKIA TAREHE 23/11/2020

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ni mojawapo ya Wilaya iliyopata ruzuku kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kidogo cha kuchakata na kufungasha asali, kiwanda hiki kinajengwa katika kata ya Katente.

Halmashauri ilisaini mkataba wa ujenzi wa kiwanda hiki kati yake na Mfuko wa Misitu Tanzania tarehe **30/05/2020** katika ukumbi wa OR-TAMISEMI jijini Dodoma na Mfuko wa Misitu Tanzania uliridhia kutoa kiasi cha Tshs **504,108,488.30/=** kwa awamu mbili, awamu ya kwanza **Tshs 296,770,306.30/=** kwa ajili ya ujenzi wa jengo na awamu ya pili **Tshs 207,338,182/=** kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kuchakata mazao ya nyuki. Fedha za awamu ya kwanza Kiasi cha **Tshs.296,770,306.30/=** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kiwanda zilipokelewa tarehe 0**5/06/2020** kwa risiti namba **633090c2001376** kupitia akaunti ya Halmashauri ya maendeleo, akaunti namba **LGA 9921210301BOT.**

### 17.3 HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MRADI.

Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 30/07/2020 ambapo kazi za awali kulingana na mpango kazi ziliweza kutekelezwa. Hadi sasa mradi uko kwenye hatua ya usawa wa lenta ya milango na mafundi wako saiti wanaendelea na kazi. Aidha malipo ya Tshs **58,921,042.92/=** zimekwishatumika na kiasi kilichobaki ni Tshs **237,849,263.38/=** kama ifuatavyo:-

**JEDWALI NA; 38 – MATUMIZI YA FEDHA**

| Na. | Tarehe | Shughuli | Kiasi kilicholipwa |
|---|---|---|---|
| 1 | 02/09/2020 | Kununua vifaa vya maji | 2,040,000 |
| 2 | 09/09/2020 | Kununua Shajala | 519,000 |
| 3 | 18/09/2020 | Kununua saruji mifuko 1200 | 22,200,000 |
| 4 | 06/10/2020 | Malipo ya awali ya fundi wa ujenzi | 4,000,000 |
| 5 | 09/10/2020 | Malipo ya vifaa vya ujenzi | 4,205,000 |
| 6 | 19/10/2020 | Kununua saruji mifuko 822 | 12,005,310 |
| 7 | 19/10/2020 | Gharama za usafiri wa saruji (822) | 3,288,000 |
| 8 | 23/10/2020 | Malipo ya vipimo | 769,820 |
| 9 | 24/10/2020 | Ununuzi wa nondo | 760,000 |
| 10 | 25/10/2020 | Safari ya kupeleka vipimo | 160,000 |
| 11 | 27/10/2020 | Malipo ya fundi awamu ya pili | 4,865,912.92 |
| 12 | 30/10/2020 | Gharama za ushushaji wa saruji (822) | 82,200 |
| 13 | 07/11/2020 | Malipo ya vibarua na ununuzi wa umeme | 260,000 |
| 14 | 17/11/2020 | Malipo ya fundi ujenzi kukamilisha boma | 3,765,800 |
| **JUMLA** | | | **58,921,042.92** |

### 17.4 CHANGAMOTO KATIKA UJENZI WA KIWANDA CHA ASALI.

i. Changamoto ya Kibajeti.

-Fedha za awamu ya kwanza zilipokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2019/2020nje ya bajeti hivyo kulazimu kuomba vifungu ndani ya mkoa ili kuwezesha vifungu vya matumizi ya fedha hivyo kufanya kuchelewa kwa mradi.

-Kufungwa kwa mifumo ya kifedha mwishoni mwa mwaka.

- Usuluhishi wa kibajeti wa fedha zilizovuka mwaka ulifanyika na kukamilika tarehe 28/08/2020 na kuruhusu kutumika kwa fedha.

### 17.5 MIKAKATI NA NAMNA YA UTATUZI WA CHANGAMOTO KATIKA UJENZI WA KIWANDA CHA ASALI

✓ Halmashauri imefanya na inaendelea kufanya jitihada ya kupata vifaa kutoka kiwandani na kwa wakala wa viwanda husika walioko kwenye mikoa kwa kuomba nukuu za bei kwa baadhi ya vifaa kama saruji ili kuweza kufanya manunuzi.

## 17.6 CHANGAMOTO ZA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI

i. Uvamizi wa misitu kwa shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa, mbao na nguzo.
ii. Kutokuwepo na kituo maalum cha kukusanyia na kuchakata na kuuza mazao ya nyuki
iii. Upungufu wa watumishi:
iv. Ufinyu wa bajeti na upatikanaji wa fedha za kusimamia raslimali misitu na ufuatiliaji wa shughuli za ufugaji nyuki
v. Mabadiliko ya tabia nchi
vi. Upatikanaji ya zana za kisasa za ufugaji nyuki na uchakataji wa mazao ya nyuki
vii. Uelewa duni wa wafugaji nyuki juu ya mbinu bora za ufugaji nyuki wa kisasa na uchakataji wa mazao ya nyuki.

## 17.3 MIKAKATI YA KUBORESHA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI WILAYANI

**i.** Kuboresha vikundi vilivyopo kwa kuviunda upya na kuvisajili ili kurahisisha utoaji wa huduma inayohitajika.
ii. Kulasimisha shirikisho la vikundi vya wafugaji nyuki ili kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma mbalimbali kwa wafugaji
iii. Kuhakikisha uwepo wa kituo maalum cha kukusanya, kuchakata na kuuzia mazao ya nyuki, na upatikanaji wa vifaa vya ufugaji nyuki wa kisasa ndani ya wilaya.
iv. Elimu endelevu kwa wafugaji nyuki ni muhimu ili kuongeza uhifadhi wa misitu na kuongeza ubora na wingi wa mazao ya nyuki.

Nwasilisha

**TAARIFA YA KITENGO CHA UCHANGUZI KWA KIPINDI KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2020**

## 18.0 UTANGULIZI

*Mhe. Mwenyekiti;*

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ni miongoni mwa Wilaya sita katika Mkoa wa Geita, zilizokuwa zinatekeleza zoezi la Uchaguzi Mkuu mwaka 2020, ambapo zoezi lilianza kwa mafunzo kwa ARO – Jimbo, ARO – Kata, hatimaye Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidzi wa Vituo na Makarani waongozaji.

Aidha vifaa kwajili ya zoezi la Uchaguzi Mkuu 2020 na vifaa vya mafunzo pamoja na mafunzo viligharamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## 18.1 IDADI YA WATUMISHI

i. Jedwali Na; 39 - Ngazi ya Jimbo jumla ya watendaji ni sita (6) walioteuliwa.

| NA. | JINA KAMILI | CHEO | UTEUZI |
|---|---|---|---|
| 1. | Dionis M. Mnyinga | DED | RO |
| 2. | Yusuph B. Mwaipalu | EO | EO |
| 3. | Leah G. Kibaki | DHRO | ARO JIMBO |
| 4. | Bernard J. Majubu | DT | ARO JIMBO |
| 5. | Patrick Ndaba | PMU | ARO JIMBO |
| 6. | Honorat S. Mtasingwa | HRO | ARO JIMBO |

ii. Watendaji Ngazi ya Kata.

Jumla ya Wasimamizi Ngazi ya Kata ni 34 waliteuliwa.

- Mabadiliko katika uteuzi Ndugu; Seni Nkuba – ARO Kata ya Igulwa alitenguliwa na kuteuliwa Joseph Msusa WEO – Igulwa.

iii. Uteuzi wa Watendaji wa Vituo

- Jumla ya Watendaji wa Vituo wakuu 471 waliteuliwa.
- Jumla ya Watendaji wa vituo wasaidizi 942 waliteuliwa
- Jumla ya Makarani 471 waliteuliwa
- Watendaji wa akiba makarani 34 na watendaji wa vituo 34

iv. Walinzi wa Vituo

- Jumla ya walinzi 471 waliteuliwa.

## 18.2 MAPOKEZI NA MATUMIZI YA FEDHA

- Fedha zilizopokelewa ni Tshs **797,928,999.87.**
- Fedha zilizotumika ni Tshs **797,928,558.5**4

**HALI YA UCHAGUZI**

**i. JEDWALI NA; 40 - WAGOMBEA WALIOCHUKUA FOMU.**

| **UBUNGE** | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **JINA** | **CHAMA** |
| 1. | RENATUS PESA NZEMO | CHADEMA |
| 2. | ANTHONY KABIKA VIGELO | CCK |
| 3. | EDWARD DEOGRATIAS KABIKA | ACT- WAZALENDO |
| 4. | DOTTO MASHAKA BITEKO | CCM |
| 5. | MIHALALO SALIM MIHALALO | TLP |

**ii. JEDWALI NA; 41 - UDIWANI**

| **NA.** | **CHAMA** | **IDADI YA KATA** |
|---|---|---|
| 1. | CCM | 17 |
| 2. | CHADEMA | 17 |
| 3. | CUF | 04 |
| 4. | NCCR – MAGEUZI | 03 |
| 5. | TLP | 02 |
| 6. | ACT – WAZALENDO | 07 |

**iii. JEDWALI NA; 42 - WABUNGE WALIOTEULIWA KUGOMBEA.**

| **Na.** | **JINA** | **CHAMA** |
|---|---|---|
| 1. | RENATUS PESA NZEMO | CHADEMA |
| 2. | ANTHONY KABIKA VIGELO | CCK |
| 3. | EDWARD DEOGRATIAS KABIKA | ACT- WAZALENDO |
| 4. | DOTTO MASHAKA BITEKO | CCM |
| 5. | MIHALALO SALIM MIHALALO | TLP |

**iv. JEDWALI NA; 43 - MADIWANI WALIOTEULIWA KUGOMBEA.**

| **NA.** | **CHAMA0** | **IDADI YA KATA** |
|---|---|---|
| 1. | CCM | 17 |
| 2. | CHADEMA | 17 |
| 3. | CUF | 04 |
| 4. | NCCR – MAGEUZI | 03 |
| 5. | TLP | 01 |
| 6. | ACT – WAZALENDO | 04 |

**Idadi ya wagombea amabao hawakuteuliwa na sababu.**

i. **UBUNGE**

Wote waliochukua fomu waliteuliwa.

ii. **UDIWANI**

TLP – Mgombea mmoja hakuteuliwa kwa sababu alijidhamini mwenyewe.

**Idadi ya Pingamizi zilizopokelewa na kuamuliwa**.

- Pingamizi moja ilipokelewa kutoka kwa mgombea wa TLP na maamuzi yaliyoamuliwa ni kwamba mgombea hakuwa na sifa ya kuwa mgombea kwa sababu alijidhamini yeye mwenyewe.

**Rufaa.**

- Hapakuwa na rufaa kutoka kwa mgombea yoyote.

**v. KAMPENI NA MAADILI YA UCHAGUZI.**

Hali ya Kampeni ilikuwa ya utulivu na amani hapakuwa na matukio yakusababisha uvunjifu wa amani au mgombea kutoendelea na mkutano.

**vi. MAWAKALA WA VYAMA VYA SIASA.**

- Jumla ya Mawakala walioapishwa ni **1,077**.

**vii. MAFUNZO KWA WATENDAJI.**

Mafunzo kwa Watendaji wote yaligharamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

viii. **VIFAA VYA UCHAGUZI**.

Vifaa vyote vilivyotakiwa katika zoezi la Uchaguzi vikiwemo vya mafunzo na vya zoezi la Uchaguzi vilipokelewa kwa wakati.

**ix. ELIMU KWA WAPIGA KURA.**

Njia zilizotumika kufikisha Elimu kwa Wapiga kura.

- Njia za magari ya matangazo, mbao za matangazo na viongozi wa madhehebu ya dini.

**x. KUPIGA KURA**

- Idadi ya waliojiajiandikisha kupiga kura ilikuwa **175,062**
- Idadi ya vituo vya kupigia kura **471**.
- Idadi ya waliopiga kura ni **131,284**
- Idadi ya kura halali ni **129,719.**
- Idadi ya Kura zilizokataliwa **ni 1,565**

Hali ya usalama siku ya kupiga kura.

- Kiujumla hali ilikuwa salama na tulivu.

**xi. MATOKEO YA UCHAGUZI**

*Mhe. Mwenyekiti;*

Katika Uchaguzi Mkuu huo, Chama cha Mapindizu (CCM) kilipata ushindi kwa asilimia 91 katika Matokeo ya Kiti cha Urais, Asilimia 85 katika Kiti cha Ubunge na katika matokeo ya udiwani, CCM kilipata ushindi katika Kata zote 17.

**xii. CHANGAMOTO KWENYE MCHAKATO MZIMA WA UCHAGUZI MKUU.**

Ufinyu wa bajeti kwenye vitu vifutavyo:-

- Mafuta.
- Shajala
- Ujenzi wa vibanda.

**xiii. MIKAKATI YA UTATUZI WA CHANGAMOTO**

Uchaguzi ujao kuongeza bajeti kwenye vitu tajwa hapo juu.

*Mhe. Mwenyekiti;*

Naomba kuwasilisha.



Dionis M. Myinga

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**BUKOMBE**